




ILANI YA UCHAGUZI MKUU 2020

#KAZINA BATA



TANZANIA YENYE UCHUMI UNAOPAA NA WATU WENYE RAHA NA FURAHA



Utangulizi	iii
1. HALI YA NCHI YETU NDANI YA MIAKA MITANO ILIYOPITA (2015 – 2020).....	1
2. UJENZI WA TAIFA LENYE MISINGI YA UHURU	7
2.1.Uhuru.....	8
2.1.2.Uhuru wa vyombo vya Habari	7
2.1.3.Uhuru wa Mihimili ya Serikali	9
2.2 Usawa.....	10
2.3. Haki.....	12
2.4. Utawala wa Sheria	14
3. UFANISI NA UBORA WA HUDUMA ZA JAMII	18
3.1. Elimu	19
3.2. Afya	22
3.3. Maji.....	24
3.4. Nishati endelevu.....	25
3.5. Hifadhi ya Jamii.....	26
3.6. Makazi Bora	27
4. UCHUMI WA WATU	28
4.1.Biashara zenye Tija na endelevu.....	29
4.2.Ajira	30
4.3.Michezo, Sanaa na Burudani	31
4.4.Kilimo, mifugo na uvuvi:	32
4.5.Kujenga Utajiri wa Jamii kupitia Ushirika wa kisasa	34
4.6.Ardhi kwa maendeleo ya Watanzania	36
4.7.Kujenga Miundombinu Wezeshi	37
4.8.Viwanda vya zana na usindikaji	38
4.9.Utajiri kwenye maliasili	38
4.9.1. Utalii	38
4.9.2. Bahari na Bandari	39
4.9.3. Madini	40
4.10 Miradi ya Kimkakati	40
4.11. Kulinda Mazingira.....	41
4.12. Sera za Kodi	42
5. GHARAMA ZA KUTEKELEZA ILANI.....	44
6. TANZANIA KUFIKIA 2025	48



UTANGULIZI



Tanzania yenye watu wenye hali bora kijamii na furaha ya kweli, yenye kujali utu, yenye mfumo mzuri wa utoaji haki, yenye demokrasia ya kweli, yenye uhuru na yenye uchumi jumuishi, imara na unaostawi” Hii ndio Tanzania itakayojengwa na kusimamiwa na Serikali ya ACT Wazalendo. Uchaguzi huu ni uchaguzi wa kuchagua.

- Uhuru wa kweli kwa kila mtu dhidi ya utumwa,
- Matumaini dhidi ya hofu,
- Amani na usalama kwa kila mtanzania dhidi ya tafrani na misukosuko
- Siasa safi dhidi ya siasa za chuki na za kizandiki
- Utaifa na mahusiano yenye tija kimataifa dhidi ya mgawanyiko na kujitenga
- Maendeleo jumuishi dhidi ya maendeleo ya wachache,
- Utajiri wa watu dhidi ya utajiri wa Serikali,
- Kuongozwa na vijana dhidi ya kutawaliwa na walewale
- Na muhimu zaidi ni uchaguzi wa kuchagua kurudisha utu na heshima kwa kila mtanzania hasa wanawake na watoto dhidi ya kejeli, manyanyaso ya makundi fulani ya jamii yetu.

ACT wazalendo imedhamiria na imejiandaa kikamilifu kujenga na kuongoza Tanzania ya Watanzania. Tanzania ambayo kila mtanzania; mtoto, kijana, mwanamke, mwanamume, mzee, wa kijijini na mjini ana haki sawa mbele ya sheria na ana fursa stahiki za kujenga na kujifikia ndoto zake. Tanzania ambayo, watanzania wanajivunia kuwa watanzania na sio Tanzania hii ya sasa ambayo mamilioni ya watanzania wanavumilia kuwa watanzania.

Chama cha ACT Wazelendo kinaamini kwa yakini, miongo inayokaribia sita tangu tupate uhuru wetu kutoka kwa mkoloni, watanzania, hawapaswi na hawastahili kuishi kwa hofu na kufifishwa ndoto zao, bali wanapaswa kuwa wenye furaha, raha, matumaini yakufia na kuishi mafanikio yao binafsi na kuwa sehemu ya mafanikio ya taifa kwa ujumla.

Serikali ya ACT wazalendo itahakikisha upatikani na ulinzi wa haki na ustawi wa watu wenye ulemavu, watoto hasa walioko kwenye mazingira magumu, jamii na makundi yaliyopo pembezoni na wanawake ambao ndiyo walezi wa taifa hili. Tafiti za kisayansi zimeonyesha na kuthibitisha kuwa kuwezesha na kuwekeza kwa wanawake na makundi mengine maalumu, kuna tija endelevu kiuchumi na kijamii. Muhimu zaidi, kunaleta umoja na usawa katika jamii. Serikali yetu sio tu itatokomeza ubaguzi ila pia itafanya jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa kila mtanzania, bila kujali jinsia, dini, maumbile, itikadi, umri, kabila, anashiriki kikamilifu katika kuongoza taifa hili katika nyanja mbalimbali na anaishi maisha yenye mafanikio, raha na furaha. Kauli mbiu yetu ya #KaziNaBata ni dhana jumuishi, kwa sababu kila Mtanzania, ana haki ya kufurahia utanzania wake, na maisha yake. Tunataka Watanzania wafanye Kazi kwa bidii na pia wafaidi matunda ya jasho lao. Wawe na Raha na Furaha.

Kwenye Taifa lenye zaidi ya 80% ya watu wake wakiwa na umri chini ya miaka 35, ni dhamira yetu, kuwekeza na kutengeza sera, sheria na taratibu zitakazohakikisha kuwa vijana wa taifa hili wanakuwa kipaumbele na chachu ya maendeleo, kwao wao na kwa taifa. Serikali ya ACT Wazelendo, imekataa kuona vijana wa taifa hili wananyang'anywa fursa, wanakatishwa ndoto zao, wanakandamizwa na kufanywa watwana ndani ya taifa lao. Serikali itakayoundwa na ACT wazelendo, itakuwa Serikali ya vijana kwa ajili ya vijana wa Tanzania wa kike na wa kiume. Lakini pia itakuwa Serikali ya kuandaa na kusimamia upatikanaji wa maisha stahiki uzeeni kwa kuwa na mfumo madhubuti wa Hifadhi ya Jamii ambao utahakikisha kuwa kila Mtanzania anakuwa na Bima ya Afya na Pansheni akifika umri wa kutoweza kufanya kazi.



Huduma za jamii bora, zenye ufanisi na zinatolewa kwa wakati stahiki hazitakuwa ni upendeleo kwa viongozi au makundi ya watu wachache, bali zitakuwa kwa kila mtanzania. Elimu bora yenye kukidhi vigezo vya soko la ajira na kuwaanda wahitimu kuvumbua na kujiajiri, huduma bora za afya, upatikaji wa maji na umeme wa uhakika na gharama nafuu ni huduma za msingi katika kuijenga Tanzania ya watanzania chini ya Serikali ya ACT Wazalendo.

Uchumi wa taifa litakaloongozwa na Serikali ya ACT Wazelendo utakuwa uchumi jumuishi, UCHUMI WA WATU SIO VITU. Uchumi wa Wananchi walio wengi na si uchumi wa Serikali na kundi la wachache. Serikali yetu itawekeza kwenye sekta zinazoajiri watanzania wengi, hasa Kilimo, Ufugaji na uvuvi, pia itaboresha na kuwezesha ustawi wa sekta isiyo rasmi hasa ya biashara ndogondogo ambazo nyingi zinafanywa na wanawake na vijana. Mifumo ya kodi na urasimishaji biashara vitalenga katika kuleta ufanisi na kukuza biashara na si kudumaza na kuleta ukiritimba. Tafiti, sayansi na tekinolojia vitakuwa chachu katika kutengeneza fursa na kukuza uchumi jumuishi. Serikali yetu itahakikisha wataalamu wa fani mbalimbali wanawekewa mazingira sawia ile walisaidie Taifa katika kukuza uchumi ambao unaboresha maisha ya mtu mmoja mmoja.

Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar utakuwa wa Usawa, wa Haki, wa Kuheshimiana na wa manufaa kwa pande nchi zote mbili zilizounda Muungano. Umoja na udugu wetu utaimarishwa kwa kuwa na Katiba mpya itakayoboresha Muundo wa Muungano. Vivyo hivyo, Serikali yetu itajikita katika kufufua na kuimarisha uhusiano wetu mataifa mengine. Tumedhamiria kurudisha heshima ya Tanzania kwenye medani ya kimataifa.

Serikali yetu ya #KaziNaBata haitaweza kufikiwa kama wasanii na wanamichezo wataendelea kunyonywa na kufanya kazi katika mazingira magumu. Kwa kushirikiana na wasanii na wanamichezo mbalimbali, Serikali yetu itawekeza kwa kiwango kikubwa kuhakikisha vipaji na vipawa vya watanzania vinakuwa vyenye tija kwao, burudani kwetu na tunu ya taifa katika majukwaa ya kimataifa. Sanaa na Michezo itakuwa ni moja ya vipaumbele ya Sera yetu ya mambo ya Nje na Biashara ya Kimataifa ili kujenga taswira chanya ya Nchi yetu na kuongeza Mapato ya Fedha za Kigeni.

Ilani hii ni dhamira ya chama katika kuifikia na kuijenga Tanzania ya watanzania, zaidi ni mkataba kati cha chama na watanzania. Hivyo basi, kwa kipindi chote cha uongozi wa Serikali ya ACT wazalendo, tutaitekeleza kwa ujumla wake, tutailinda na kuiheshimu. Ilani hii imetengenezwa kutokana na maoni, matarajio na matakwa ya watanzania yaliyotolewa kwa maandishi kupitia kamati ya ilani na kwenye ziara mbalimbali za viongozi wa chama. Pia maoni yaliyokusanywa kwenye Ziara za kuwasikiliza Wananchi zilizofanywa na Chama tangu mwaka 2019.

Sisi, ACT Wazalendo tunaamini na tunawataka wataanzania waamini pamoja nasi kuwa, INAWEZEKANA.

- Kufanya kazi na kula bata
- Kuishi maisha ya raha na furaha
- Kuondoa Serikali dhalimu madarakani
- Kuwa na Serikali inayoheshimu sheria, utu, uhuru na ustawi wa watu wake
- Kujenga uchumi jumuishi na endelevu
- Kila mtanzania kufikia ndoto zake
- Kuwa na umoja wa kitaifa na heshima kimataifa
- 2020 ni muda sahihi kwa wataanzania kuchagua Serikali mpya ya inayoundwa na viongozi na watu watakaoweza kubuni na kutekeleza sera zitakazowaondolea wananchi Hofu, Adha, Ufukara na kuwapa Maisha yenye Raha na Furaha. #KaziNaBata

Zitto Zuberi Kabwe

Kiongozi wa Chama

Agosti 2020



1. HALI YA NCHI YETU NDANI YA MIAKA MITANO ILIYOPITA (2015 – 2020)

Katika miaka mitano iliyopita, nchi yetu imepitia na inaendelea kupitia misukosuko mingi mikubwa iliyosababishwa na utawala wa kikandamizaji wa Chama Tawala. Wananchi wengi wamejikuta ni wahanga wa misukosuko hiyo, kwa namna moja au nyingine. Makundi mbalimbali, kama si yote, ya jamii yetu yameumizwa na maamuzi, sera na matendo ya watawala wa nchi yetu.

Msukosuko wa kwanza na mkubwa ni upotevu wa uhuru na haki. Uhuru wa kujieleza, uhuru wa vyombo vya habari, haki ya kujumuika na haki ya kukosoa zote zimeporwa na watawala. Ndani ya miaka mitano hii tumeona wananchi tukigawanywa kidini, kikabila na kwa itikadi za vyama vyetu. Umeona utawala wa sheria ukipuuzwa, mchakato wa Katiba Mpya ukisitishwa, na sheria mbaya za kulinda viongozi na zisizo na tija kwa ustawi wetu zikipitishwa bila woga.

Vilevile, ni miaka mitano iliyotumika kuingilia mgawanyo wa madaraka baina ya Mihilimili ya dola na kuvunja taasisi zote za uwajibikaji nchini, na hivyo kutoa mwanya wa mapato ya umma kutumika vibaya bila usimamizi, huku demokrasia ya vyama vingi ikiminywa zaidi na kuzima kila sauti na mawazo mbadala.

Wakosoaji wa watawala wamekumbana na mateso na ukatili wa hali ya juu, wapo waliouawa, wapo waliotekwa au kupotea na hadi leo hatujui walipo, wapo waliomiminiwa risasi kwenye maeneo ya Bunge na hadi leo hakuna hatua zilizochukuliwa, wapo ambao ofisi zao zilipigwa mabomu, wapo waliobambikiziwa kesi kwa mashtaka yasiyo na dhamana, hasa yale ya utakatishaji fedha na uhujumu uchumi ili kunyamazishwa, na wapo ambao wanaendelea kupandishwa kwenye vizimba vya mahakama kila uchao ili kuwadhibiti wasiweze kufanya shughuli za kisiasa kwa uhuru. Kwa mujibu wa Kituo cha Haki za Binadamu nchini (LHRC), asilimia hamsini na nne (54%) ya watu wote walioko magerezani mwaka 2019 ni mahabusu ambao husababisha msongomano uliokithiri kwenye magereza. Kimsingi, hawa ni Watanzania, wanaotumikia adhabu kabla ya kuhukumiwa.

Demokrasia imezorota kwa kiwango kisichofikirika, chaguzi ndogo zilizosababishwa na ununuzi wa wabunge wa upinzani ziliendeshwa kwa uporaji, vitisho na hadaa. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 ulitoa picha iliyo sahihi kuwa, kwa sasa, Tanzania si nchi inayoheshimu misingi ya demokrasia na utawala bora. Kwa mfano, asilimia tisini na sita (96%) ya wagombea wote wa chama chetu cha ACT Wazelendo walienguliwa kushiriki uchaguzi huu, kitu kilichopelekea vyama vya siasa vya upinzani kujitoa kushiriki uchaguzi. Leo hii kwa kigezo cha Serikali za Mitaa, Nchi yetu ni ya Mfumo wa Chama kimoja cha Siasa, kwani Serikali zote za Vijiji, Vitongozi na Mitaa zinashikwa na watu kutoka chama kimoja.

Ni miaka mitano iliyorudisha nyuma shughuli za kiuchumi za asilimia sabini na mbili (72%) ya wananchi, wakulima walidhulumiwa fedha zao ama kupata hasara kwa sababu ya sera mbaya na taratibu za hovyzo zilizoathiri soko la mazao yao, iwe ni wakulima

wa mazao ya biashara kama Korosho, Pamba na Tumbaku, au wa mazao ya chakula kama Ufuta, Mbaazi na Mahindi. Miaka mitano hii ni kipindi ambacho tulishuhudia wavuvi wakichomewa nyavu zao, kuanzia pwani ya Bahari ya Hindi mpaka kwenye mito na maziwa yetu, huku wengi wao wakifungwa au kupigwa faini kubwa na Mahakama zinazotembea na zinazoendeshwa na Serikali. Na pia imekuwa miaka mitano ya mateso kwa wafugaji waliotaifishiwa mifugo yao bila kuwezeshwa kupata ardhi yenye rutuba na maji ya kuchunga mifugo hiyo. Wakulima, wavuvi na wafugaji wamefukarishwa mno.

2015 - 2020 ni miaka mitano ya kutumikishwa tu bila tija. Hamasa na motisha kwa wafanyakazi nchini haipo tena, maana wafanyakazi hawakupipwa stahiki zao, hawakupata nyongeza ya mishahara yao, na wale waliostaafu wameendelea kucheleweshewa pensheni zao. Wafanyabiashara nchini wameathirika zaidi. Serikali iliamua kwa makusudi kufanya biashara yenyewe kwa yenyewe, ikiondoa ushindani na kuyabeba mashirika na taasisi zake tu hata kwenye sekta ambazo wafanyabiashara binafsi nao wamewekeza, kuanzia Bima, Usafiri, Ujenzi mpaka Mawasiliano.

Ni wakati ambao wafanyabiashara walibambikiwa kodi za kufikirika, jambo lililosababisha biashara nyingi kufungwa na ajira kupotea. Wakandarasi wa ndani wachache wanaoshiriki kutelekeza miradi mbalimbali hawalipwi fedha zao kwa wakati, jambo linalopelekea kuharibu zaidi mwenendo wa mzunguko wa fedha kwenye Uchumi. Wamiliki wa viwanda na wauzaji wa bidhaa kwenda nje wanaidai Serikali zaidi ya Shilingi Trilioni 2 za malimbikizo ya ritani za kodi na kusababisha shughuli za uzalishaji kudorora kwa sababu ya matatizo ya mzunguko wa fedha 'cashflow'. Viwanda vingi vimepunguza wafanyakazi na kusababisha maisha magumu sana kwa Watanzania.

Ni miaka mitano ya huduma mbaya za jamii, elimu ya msingi na sekondari ikitolewa bila malipo lakini isiyo na ubora, kukiwa na uhaba mkubwa wa vyumba vya madarasa na madawati, uhaba wa walimu na mazingira mabaya ya kufanyia kazi na kuishi walimu. Elimu ya Ufundi ikipuuzwa, na hivyo kulinyima taifa rasilimali watu ya mafundi mchundo wa kusukuma uchumi wa viwanda. Zaidi ya hayo, elimu ya juu imesuasua kwa mikopo michache yenye ubaguzi, isiyotolewa kwa wakati na inayowazalishia wahitimu wetu mzigo wa madeni yasiyolipika huku wakiwa hawana uhakika wa ajira baada ya kuhitimu.

Huduma ya maji safi na salama bado iliendelea kuwa tatizo kuu katiba miaka mitano hii, hasa vijijini, huku kukiwa na miradi mingi inayotajwa kukamilika lakini isiyotoa maji kabisa, na hivyo wananchi wanaendelea kusumbuka kuyatafuta maji pamoja na kupata maradhi mbalimbali yatokanayo na matumizi ya maji yasiyo safi na salama.

Huduma kwenye sekta ya afya nazo hazikusalimika na misukosuko, kuanzia uhaba wa majengo, uchache wa watumishi na ukosekanaji wa vifaa tiba, huku wananchi wengi wakikosa hata uwezo wa kuchangia huduma hizo. Sehemu ya pato la taifa (GDP), inayotengwa kwa matumizi ya afya, imepungua kutoka 8% mwaka 2006 hadi 1% mwaka

2019. Hiki ni kiwango kidogo kulinganisha na lengo la 15% lililokubaliwa na nchi za Umoja wa Afrika (Azimio la Abuja 2001). Ongezeko la vituo vya huduma za afya (zahanati, vituo vya afya na hospitali) halikidhi mahitaji ya Watanzania. Serikali ya awamu ya tano imeongeza sehemu za kutolea huduma za afya 1,585 ndani ya miaka mitano, ikiwa ni sawa na 16% tu ya mahitaji ya ujenzi wa wastani wa vituo 2000 kila mwaka, ili walau kuweza kufikia mahitaji ya ongezeko la idadi ya watu kila mwaka. Hadi sasa kuna vituo vya huduma za afya 9,104 ambavyo ni asilimia kumi na sita (16%) ya mahitaji ya vituo 55,000 nchi nzima. Afya imekuwa ni bidhaa kama ilivyo bidhaa nyingine zenye kuuzwa na kununuliwa kwenye soko huria, mwenye pesa na mamlaka hupata bora na zaidi na wale wasio na uwezo huambulia huduma hafifu au kukosa kabisa.

Ni miaka mitano ambayo Serikali imeendelea kuchukua mikopo, yenye riba kubwa. Pia Serikali imeanzisha miradi mikubwa kama vile reli ya kati ya kisasa (SGR), bwawa kubwa la kufua umeme (Stigler's Gorge), na ununuzi wa ndege, inayoendelea kutekelezwa ama kwa fedha za ndani au mikopo ya kibiashara ya muda mfupi, hivyo, kuleta madhara kwenye uchumi. Mikopo hii ya kibiashara inakuza ukubwa wa deni la taifa na kuongeza gharama za kuhudumia deni hilo kwa kuzitoa fedha nchini na kulipa madeni nje. Kibaya zaidi miradi hii ni miradi isiyo na fungamanisho na bidhaa zinazozalishwa nchini, na hivyo vifaa, vipuri na ufundi wa miradi vyote vikinunuliwa kutoka nje, hivyo kutokuwa na mnyororo mrefu wa kiuchumi kwa Watanzania.

Deni la Taifa limeongezeka kwa kasi kubwa sana. Serikali ya awamu ya nne ilipoingia madarakani mwaka 2005, deni la nje lilikuwa dola za Marekani bilioni nane (\$8 bn), na ilipoondoka mwaka 2015 deni hilo lilikuwa limefikia dola za Marekani bilioni kumi na tano (\$15 bn), hii ni sawa na ongezeko la deni la nje la dola za Marekani bilioni 7 ndani ya miaka kumi. Hata hivyo, mpaka kufikia mwezi Machi mwaka 2020, deni la nje limefikia dola za Marekani bilioni 22.4 sawa na ongezeko la dola za Marekani bilioni 7.4 katika kipindi cha miaka 5 hii ya sasa. Yaani Serikali ndani ya miaka hii mitano, imekopa zaidi ya mikopo yote ambayo Serikali ya awamu nne ilichukua katika miaka 10 ya uongozi wake.

Athari ya ukopaji huo mkubwa ndani ya miaka hii mitano tayari inaonekana sasa, gharama za kulipa madeni zimeongezeka kwa 8% kati ya mwaka 2019/20 – 2020/21, wakati ongezeko la mapato ya ndani ya Serikali ni 6% tu. Iwapo miradi inayosababisha nchi kukopa haitaweza kuzalisha mapato ya kugharamia malipo ya madeni, basi ni dhahiri Serikali italazimika kuondoa fedha kwenye huduma muhimu kama Elimu, Maji na Afya na kuzielekeza kulipa madeni, na hivyo kupelekea huduma hizo za jamii, ambazo tayari zina hali mbaya, kuzorota zaidi. Katika Bajeti ya mwaka 2020/2021, Bajeti ya kulipa deni na mishahara ni 79% ya mapato yote ya ndani ya Serikali.

Mwisho na muhimu zaidi, 2015-2020 imekuwa miaka mitano yenye mateso na manyanyaso kwa wanawake. Hedhi inatozwa kodi, na wahanga wa mimba za utotoni wameendelea kunyimwa haki yao ya kupata elimu. Serikali haikuwalinda wanawake kwa matamko na kwa vitendo, jambo lililochangia kuongezeka kwa matukio ya ukatili wa kijinsia. Takwimu za karibuni zinaonyesha matukio 88,612 yameripotiwa kati ya mwaka 2017 na mwaka 2019. Matukio ya ubakaji na ulawiti wa watoto yaliripotiwa yameongezeka kutoka 759 mwaka 2017 mpaka matukio 4,397 mwaka 2019. Na katika hali ya kuhuzunisha, uongozi umekuwa ni haki kwa wanaume tu, kwa mfano, kuna wanawake wanne tu kwenye baraza la mawaziri linalomaliza muda wake, sawa na asilimia ishirini (20%) ya mawaziri wote, ukilinganisha na mawaziri wanawake 11 sawa na asilimia thelathini na sita (36%) kwenye Serikali ya awamu nne. Hali ni mbaya zaidi katika nafasi nyingi za kuteuliwa, kimsingi, teuzi za Serikali inayomaliza muda zimekuwa #TeuziDume.

MUHTASARI WA VIPAUMBELE

#KAZINABATA



Ujenzi wa Demokrasia
na Utoaji Haki za
Watu



Ufanisi na Ubora wa
Huduma za Jamii



Uchumi wa Watu



Uhuru kwa kila Mtu



Elimu Bora ya
kivumbuzi bila malipo



Kilimo cha kimapinduzi
na Mazingira wezeshi ya
Biashara



Usawa na ustawi wa
wanawake na vijana



Hifadhi ya Jamii kwa
Kila Mtu/Afyu Bora kwa
wote



Ushirika wa kisasa kwa
Maendeleo Jumuishi



Haki za watu wenye
ulemavu



Maji safi, salama na
gharama nafuu



Ajira Mpya
Milioni 10



2. UJENZI WA TAIFA LENYE MISINGI YA UHURU, USAWA, HAKI, UTAWALA WA SHERIA, UWAJIBIKAJI NA DEMOKRASIA



2.1. Uhuru

Watanzania hawakupigania uhuru kutoka kwa mkoloni ili waje watawaliwe kikoloni kwa kigezo cha 'kuleta maendeleo'. Uhuru wa kila Mtanzania, ni haki na msingi wa taifa la Tanzania. Kwetu sisi ACT wazalendo, hilo halina na halitakuwa na mjadala.

2.1.1. Uhuru wa kutoa maoni:

Haki na Uhuru wa kila Mtanzania kutoa maoni na kujieleza, itatekelezwa na kulindwa kwa kiwango cha juu kabisa. Ndani ya siku 100 za kwanza tangu kuingia madarakani, Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itafuta Sheria zote zinazobana, kuminya na kuffisha haki na uhuru wa Watanzania kujieleza na kutoa maoni, zikiwemo, Sheria ya Makosa ya Mtandao, Sheria ya vyombo vya habari, Sheria ya Takwimu, kanuni ya maudhui ya mtandao na sheria nyingine kandamizi.
- ii. Itatengeneza majukwaa, mifumo na kurasimisha taratibu zitakazowawezesha Watanzania kutoa maoni yao na kujieleza, kuanzia ngazi za vijiji mpaka Serikali kuu. Hii ni pamoja na kuimarisha uratibu wa uendeshaji mikutano ya vijiji, vitongoji, mitaa, kata, utaoji maoni ya wadau kwenye miswada mbalimbali bungeni na kwenye mabaraza ya Serikali za Mitaa, nk.

2.1.2. Uhuru wa vyombo vya Habari:

Katika Nchi itakayoongozwa na ACT Wazalendo, vyombo vya habari vitakuwa 'Mhimili wa Nne wa Dola', lengo ni kutoa nafasi kwa vyombo vya habari kusaidia kuonyesha mapungufu ya uongozi wetu, na kutupa nafasi ya kujirekebisha, ili kuwahudumia wananchi kwa ufanisi zaidi. Serikali ya ACT Wazalendo, ndani ya MIEZI SITA ya kwanza itafanya yafuatayo;

- i. Itafuta sheria zote kandamizi na zinazopora uhuru wa vyombo vya habari, na kutengeneza sheria, kwa kushirikiana na wadau, zitakazolenga kuleta uhuru na weledi na ukuaji wa sekta ya habari.
- ii. Itaunda Kamisheni ya vyombo vya habari ambayo itaratibu sekta ya habari na maadili ya vyombo vya habari. Kamisheni hii itakuwa huru, na yenye kujitegemea, Serikali itakuwa ni mmoja tu ya wadau wa kamisheni lakini si miliki wa kamisheni hii.
- iii. Itahakikisha vyombo binafsi vya habari vinakuwa na haki sawa ya kupatiwa taarifa na kuripoti habari kutoka Serikalini.

- iv. Itahakikisha vyombo vyote vya habari, vya umma na vya binafsi, vinakuwa na haki sawa ya kupatiwa matangazo ya Serikali.
- v. Itahakikisha vyombo vya habari vya umma vinakuwa huru kutoa taarifa yoyote kwa maslahi ya umma bila kuingiliwa au kushawishiwa na chama kilicho madarakani.
- vi. Itaunda Tume maalum kutoa mapendekezo ya kuratibu na kusimamia ajira kwenye sekta ya habari na sanaa. Kila mwandishi wa habari atakuwa na mkataba wa ajira - kwa namna itakavyopendekezwa na tume, na waajiri watalazimika kuhakikisha kila mwandishi anapatiwa Hifadhi ya Jamii na Bima ya Afya.
- vii. Itahakikisha vyama vya wanahabari vinawezeshwa kusimamia haki na maslahi ya wanachama wao bila hofu wala woga.

2.1.3. Uhuru wa Mihimili ya Serikali:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo ndani ya ndani ya miezi sita (6) ya kwanza;

- i. Itaimarisha na kusimamia uhuru wa mihimili mitatu ya Dola ili kuhakikisha kuwa inatimiza wajibu wake kwa mujibu wa sheria na Katiba ya nchi yetu.
- ii. Itatekeleza Sheria ya uendeshaji wa Bunge na Sheria ya Mahakama kwa kuwa na Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Mahakama, mifuko ambayo bajeti yake itapaswa kuwasilishwa Bungeni na Mihimili hiyo kwa ukamilifu na kwa wakati, na kutengewa fedha kama zilivyopitishwa na Bunge.

2.1.4. Uhuru wa Kukusanyika:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itasimamia uhuru na haki ya mtu mmoja mmoja, Asasi za Kiraia, Jumuiya za kijamii na Kitaaluma, pamoja na makundi mbalimbali ya jamii kukutana, kuungana, kushirikiana na kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na miongozo yao bila kuvunja Katiba ya nchi.
- ii. Itafanyia marekebisho sheria kandamizi ya Jeshi la Polisi Tanzania na huduma saidizi sura ya 322, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 kifungu cha 43 (3), (4), na (6), inayotoa mwanya wa wazi kwa polisi kuzuia uhuru wa kujumuika bila sababu yoyote ya msingi, hivyo kukengeuka Katiba yetu ya nchi ya 1977 ibara ya 20 (1) inayoruhusu Uhuru wa Kukusanyika,
- iii. Itafuta sheria na miongozo inayonyima uhuru Asasi na makundi ya kiraia kufanya shughuli zao.



2.2. Usawa

Chama cha ACT Wazalendo, kinaahidi kuijenga Tanzania inayotumia rasilimali za nchi kwa usawa bila ubaguzi wa kikabila, kikanda, kimkoa kiitikadi, kidini wala kisiasa.

2.2.1. Usawa mbele ya sheria:

Serikali ya ACT Wazalendo itahakikisha kila Mtanzania ana haki na wajibu sawa mbele ya sheria bila kujali cheo, jinsia, hali, dini, kabila wala itikadi ya siasa. Shabaha ni kuwa Taifa la Tanzania lenye haki na usawa kwa kila raia.

2.2.2. Usawa katika utoaji wa huduma:

Serikali ya ACT Wazalendo itahakikisha kuwa kutakuwa na usawa katika utoaji wa huduma za jamii na maendeleo. Kwa kuamini kwamba, maendeleo ya nchi yetu yanachangiwa na wananchi kwa kulipa kodi kwa usawa.

2.2.3. Usawa wa Kijinsia:

Ustawi wa jamii yoyote ile unatokana na kuheshimu usawa wa kijinsia. ACT Wazalendo inaamini kuwa, Taifa letu haliwezi kuendelea kama nusu ya watu wake wanabaguliwa kwa sababu ya jinsia zao. Ili kuleta usawa wa kweli wa kijinsia, Serikali ya ACT Wazalendo itasimamia utekezaji wa sheria zote za ndani ya nchi zinazohusu masuala ya jinsia na mikataba yote ya kimataifa kama CEDAW, Azimio la Maputo, Beijing Platform of Action, CPD, n.k. Pia Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itahakikisha ushiriki wa 50 kwa 50 katika ngazi zote za uongozi, hasa kwenye nafasi za kuteuliwa.
- ii. Itarekebisha sheria za mifumo ya uwakilishi wa wanawake hasa bungeni (Viti maalumu), ili kuleta mfumo utakaokuza na kuboresha ushiriki wa wanawake katika Bunge hasa kutoka kwenye majimbo.
- iii. Itawekeza katika mifumo itakayowezesha wanawake kuwa wafanyabiashara wakubwa, na wamiliki wa mifumo ya uzalishaji mali na ajira, ili kuondokana na dhana kuwa wanawake ni watu wakufanya shughuli ndogo ndogo za uchumi. Ili kufikia hilo, Serikali itaweka mifumo thabiti kuhakikisha angalau asilimia thelathini (30%) ya manunuzi yote ya ndani yatakayofanywa na Serikali kuu na Serikali za mitaa, yatatoka kwenye biashara zinazozomilikiwa na wanawake.
- iv. Itaondoa kodi na kuwezesha upatikanaji bure wa bidhaa za hedhi katika shule za msingi na sekondari Tanzania nzima.

- v. Itakomesha ukeketaji wa wanawake na watoto wa kike. Aidha, Serikali yetu itahakikisha utekaji unamalizika ndani ya miaka 10, kama ambavyo mpango wa malengo endelevu ya dunia unavyoelekeza.
- vi. Itadhibiti mimba za utotoni kwa kuhakikisha watoto wote wa kike wanapata elimu katika mazingira salama na kuhakikisha elimu rika inatolewa kwa ubora katika taasisi zote za elimu nchini ili kuwajengea uwezo watoto wa kike na wa kiume kuepuka na kutoa taarifa za unyanyasaji wa kingono. Zaidi, itahakikisha utekelezaji wa sheria zinazolinda watoto dhidi ya ubakwaji pamoja na unyanyaswaji wa kingono kwa ujumla, kwa kuwezesha jamii na Jeshi la Polisi kuwa walinzi wa haki za watoto na pia kuwajengea uwezo Jeshi la Polisi pamoja na Mahakama, kushughulikia kwa haraka kesi zinazohusu ubakaji wa watoto. Serikali yetu itaweka hadharani 'orodha ya waliotiwa hatiani kwa kubaka na kunyanyasa kingono wanawake na watoto'.
- vii. Itatoa elimu sahihi na huduma rafiki za afya ya uzazi kwa vijana, hasa wa kike walioko shuleni na nje ya shule, kwa kushirikiana na asasi za kiraia na Taasisi za Afya, Serikali itahakikisha inawafikia watoa elimu ya afya ya uzazi wa jadi na kuwajengea uwezo ili waweze kutoa elimu sahihi.
- viii. Itasimamia haki ya kupata elimu kwa wahanga wa mimba za utotoni, kwa kuhakikisha kila mtoto wa kike aliyepata mimba akiwa shule anamaliza elimu yake kama ilivyokusudiwa.
- ix. Itapitia na kufuta sheria za kimila vinazomnyima mwanamke haki ya kumiliki mali na ardhi, shabaha ni kuwa na usawa wa kumiliki mali, na ardhi kwa wanawake.
- x. Itasimamia uwepo wa usawa katika malezi ya watoto, hasa baada ya wazazi kutengena au pale watoto wanapozaliwa nje ya ndoa.
- xi. Itakomesha ukatili dhidi ya wanawake na watoto, hasa ukatili wa kingono, kimwili na udhalilishaji kwenye mitandao. Hilo litawezekana kwa kuboresha madawati ya jinsia, kuweka mifumo rahisi ya kuripoti na kudhibiti ukatili, kuunda tume maalumu ya kudhibiti ukatili wa kijinsia na kuhakikisha vyombo vya mahakama vinawezeshwa kimafunzo na kimfumo ili kusimamia kesi za ukatili kwa haraka na uhakika.
- xii. Itaendesha kampeni nchi nzima kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia katika kuondoa mila potofu.
- xiii. Itawezesha kuundwa kwa Baraza la Kitaifa la Wanawake litakalosimimia mustakabali na maendeleo ya wanawake Tanzania.



2.3. Haki

Serikali ya ACT Wazalendo itatekeleza kwa vitendo Sheria, Kanuni na Mikataba yote ya kimataifa inayolinda na kuhifadhi haki za binadamu. Pia Serikali yetu itatengeneza na kuweka mifumo maalumu ya kukusanya takwimu na kuripoti utekelezaji na upatikanaji wa haki za binadamu kwa ushirikiano wa karibu wa Asasi zisizo za KiSerikali na taasisi za kitaifa na kimataifa.

Katika kuhakikisha kuwa haki inatendeka, ndani ya Siku 100 za kwanza za uongozi wa Serikali chini ya ACT Wazalendo itaundwa Tume ya Majaji itakayochunguza vitendo vyote vya Utekaji, Watu kupotea na mauaji yote yaliyotokea kati ya mwaka 2015-2020 na kuchukua hatua za kisheria kwa wote watakaokutwa na makosa vile vile kulipa fidia kwa familia zote zitakazokuwa zimeathiriwa na vitendo husika.

2.3.1. Haki ya kupata habari:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo ili kuhakikisha uwepo wa haki ya kupata habari;

- i. Itaboresha ushiriki wa Tanzania katika mpango wa Afrika kujitathmini kiutawala bora (APRM).
- ii. Itairudisha Tanzania katika uanachama Mpango wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP), ili kuhakikisha Serikali inaendeshwa kwa uwazi mkubwa na kila Mtanzania anapatiwa haki yake ya kupata habari sahihi kwa wakati sahihi.
- iii. Itarudisha matangazo ya moja kwa moja ya Bunge (bunge live) – na kuwa na idhaa ya mtandaoni (Online Channel) ya Bunge, ili kuhakikisha wabunge wanapata nafasi ya kutosha kufafanua hoja zao kwa kina hata nje ya vikao vya Bunge.
- iv. Itafanyia marekebisho makubwa ya Sheria zinazotumika kuendesha Serikali, ili kuhakikisha mikataba yote ya miradi yenye maslahi mapana ya Taifa, kama madini, kandarasi, miradi ya ujenzi itawekwa wazi.

2.3.2. Haki ya kushiriki katika kufanya maamuzi:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itashirikisha kikamilifu wananchi kwenye kufanya maamuzi ya kila jambo ambalo lina maslahi mapana kwa Taifa, aidha kwa kupigia kura moja kwa moja, au kutoa maoni yao kwa njia ya maandishi (petition), au kupitia wawakilishi wao wa majimbo (Wabunge au Wawakilishi kwa Zanzibar).

- ii. Itatengeneza mfumo wa kisheria wa kuwalazimisha viongozi mbalimbali, aidha, kujadili, kutoa ufafanuzi au kufuta maamuzi pale idadi stahiki ya watanania watakapotaka iwe hivyo kupitia maoni ya wazi (public petition).
- iii. Itaweka kisheria utaratibu wa wananchi wanaoishi kwenye maeneo yenye rasilimali kutoa idhini ya miradi ya uvunaji wa rasilimali hizo kuanza kutekelezwa (Free Prior Informed Consent).

2.3.3. Haki za watu wenye ulemavu:

Serikali ya ACT Wazalendo, itaweka kipaumbele katika kuhakikisha haki za watu wenye ulemavu zinalindwa, kuhifadhiwa na kuhamasishwa kwa kufanya yafuatayo;

- i. Itaweka taarifa zote muhimu za umma kwenye mifumo sahihi na wezeshi kwa watu wenye ulemavu, kwa mfano, kutafsiriwa kwa lugha ya alama na nukta nundu.
- ii. Itasimamia utekelezaji wa sheria ya majengo ili kuhakikisha majengo yote ya umma yanafikika kwa urahisi kwa watu wenye ulemavu.
- iii. Itahakikisha watu wenye ulemavu wote nchini wanapata fursa sawa za kujifunza na kupata ajira stahiki katika fani na sekta mbalimbali, hii ni pamoja na kuwekeza kwenye vifaa maalumu na vya kisasa vya kujifunzia kwenye shule maalum za watu wenye ulemavu.
- iv. Itahakikisha sekta binafsi na asasi za kiraia zinatekeleza programu maalumu ya 'kuwezesha watu wenye ulemavu' kushiriki kikamilifu katika nyanja zote za jamii na kuhakikisha wanapata hifadhi ya jamii.
- v. Itahakikisha upatikanaji wa uwakilishi wa haki na wenye tija wa watu wenye ulemavu katika uongozi, ngazi za maamuzi na shughuli za kuingiza kipato.
- vi. Itahakikisha wasichana na wanawake wenye ulemavu wa viungo na wanaoishi kwenye mazingira magumu wanapatiwa bidhaa za hedhi bure.
- vii. Itahakikisha kaya maskini na zinazosimamiwana wanawake na kulea watoto wenye ulemavu watapatiwa pesa za kujikimu kila mwezi kutoka kwenye mfuko maalumu wa 'kuwezesha watu wenye ulemavu'.
- viii. Itahakikisha ulinzi wa watu wenye ulemavu dhidi ya unyanyasaji, ukatili na dhuluma.



2.4. Utawala wa Sheria

Hakuna na hakutakuwa na aliye juu ya sheria kwenye Serikali itakayoongozwa na ACT wazalendo. Kila kitu katika Serikali yetu kitaongozwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizoanishwa na vyombo mahususi vyenye mamlaka hiyo. Sheria za nchi, Serikali na taasisi zake zitalenga kuhakikisha kwamba kila raia anapata haki sawa bila kubaguliwa.

2.4.1. Katiba Mpya:

Serikali itakayoongozwa na ACT Wazalendo na vyama washirika, ndani ya miaka miwili, itafufua na kukamilisha mchakato wa kuandika Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano kwa kuwashirikisha Watanzania kikamilifu. Katiba mpya itaainisha;

- i. Itaboresha Muundo wa Muungano ili kuwa na Muungano wa Usawa, wa Haki na wenye Kuheshimiana, na kusimamia uundwaji wa muundo wa Serikali tatu.
- ii. Itaaainisha na kuimarisha misingi ya haki na usawa kisheria, na kuweka nyenzo madhubuti za kusimamia haki, usawa, na uhuru kwa raia wake.
- iii. Itaimarisha uhuru na uimara wa mihimili yote ya Serikali.
- iv. Itajali maslahi mapana ya Taifa letu na kuimarisha uwajibikaji.
- v. Itasimamia uwepo wa ‘Serikali ya Umoja wa Kitaifa’ badala ya kulimbikiza viongozi wa chama kimoja.
- vi. Italeta mfumo bora wa kuendesha Serikali hasa za mitaa – kwa kuwezesha ugatuaji (madaraka zaidi kwa Serikali za Mitaa badala ya Serikali Kuu).
- vii. Itawapa wananchi haki ya kuchagua wakuu wa mikoa kuanzia uchaguzi mkuu wa mwaka 2025
- viii. Itatoa haki kwa Watanzania kuwa na Uraia Pacha.
- ix. Itatengeneza dira ya Tanzania ya miaka mia moja inayokuja.

2.4.2. Muunganano wenye Usawa, haki, kuheshimiana na wenye mwafaka

Kumekuwa na changamoto katika kuendesha Muungano wetu baina ya Nchi mbili, Tanganyika na Zanzibar. ACT Wazalendo inaona kunahitaji kuwa na mwisho wa manung’uniko, mivutano na athari zinazotokana

na kutokuwa na mwafaka, wa namna Muungano wetu unapaswa kuwa na kudumishwa. Serikali ya ACT Wazalendo itafanya mambo yafuatayo ili kuleta Muungano wenye Usawa na haki;

- i. Kufuatia Katiba mpya ya Muungano, itahakikisha kuwa kunatungwa sheria zitakayoendana na mahitaji ya wakati chini ya msingi wa haki, heshima na usawa kama nchi mbili huru zilizoungana kwa hiari zao, ili kuwa na muungano wa haki, uwazi na usawa kwa kufaidisha kila upande
- ii. Itahakikisha kwamba mapendekezo ya tume ya pamoja ya fedha yanatekelezwa ikiwemo kuanzishwa na kufanyia kazi haraka Akaunti ya Pamoja ya Fedha. Aidha, Serikali yetu ya muungano itailipa malimbikizo yote ya haki za mapato ya Zanzibar kutokana na mapato ya ziada ya Muungano kama ilivyochambuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha. Kupitia sheria itakayotungwa na Serikali ya ACT wazalendo, kila Mwaka Serikali ya Muungano itailipa Zanzibar TShs Bilioni 660 (Transfer to Zanzibar as a payment of its accumulated non payments of its share from Union revenues).
- iii. Itaanzisha mchakato ya kurejesha mamlaka kwa Serikali ya Zanzibar katika nyenzo muhimu za uchumi ikiwemo kodi, fedha, ushirikiano wa kimataifa kwa mambo yasiyo ya Muungano, ili Zanzibar iweze kujenga uchumi imara unaoendana na mazingira na mahitaji ya uchumi na pia kuamua mustakbali wao.
- iv. Itairejeshea Zanzibar hadhi yake ya kuwa na dhamana na jukumu la kuamua juu ya masuala ya sera za kiuchumi ikiwemo pia kuratibu masuala ya mitaji ya uwekezaji. Hii itafanya Zanzibar kuwa na mipango ya uhakika ya kiuchumi, kifedha na uwekezaji.
- v. Itahakikisha kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaipatia Zanzibar mgao wake wa kifedha wa asilimia 11.02 kama ilivyowekeza katika mtaji wa uanzishwaji wa Benki Kuu ya Tanzania.

2.4.3. Kuboresha taasisi za usimamizi na Ulinzi wa Sheria:

Serikali ya ACT itafanya yafuatayo;

- i. Itaboresha muundo na utendaji wa vyombo vya dola ili kuviwezesha kufanya kazi zake kwa uhuru bila kuingiliwa kisiasa na kutekeleza majukumu yake kwa kufuata sheria na Katiba.
- ii. Itaboresha mazingira ya kufanyia kazi, makazi, na malipo ya watumishi wa vyombo vyote vya kutoa haki nchini.

2.4.4. Sheria zenye tija kiuchumi:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Italeta mfumo wa kisheria utakaondoa msururu wa kodi kwa wafanyabiashara wadogo, wa kati, na wakubwa kulingana na fursa na mahitaji yao.
- ii. Itawezesha kisheria mfumo utakaotoa nafuu ya kikodi kwa uwekezaji katika sekta zinazogusa wananchi wengi zaidi kama kilimo, ufugaji na uvuvi.
- iii. Itaondoa sheria na kanuni zote zinazoondoa uwezo wa vijana kujiajiri, hasa katika Sekta ya Habari, mawasiliano na Usafirishaji.

2.4.5. Uwajibikaji:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itaimarisha taasisi za kusimamia uwajibikaji kama Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAOT), Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) kwa kuhakikisha mchakato wa uteuzi wa wakuu wa Taasisi hizo unaidhinishwa na Bunge baada ya uteuzi wa Rais.
- ii. Itahakikisha uhuru wa taasisi za kusimamia uwajibikaji nchini.
- iii. Itahakikisha haiwavumilii viongozi wote ambao ni kikwazo kwa uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi.
- iv. Itasisitiza uwazi wa taarifa kwenye mikataba yote mikubwa ili kuwezesha taasisi zinazosimamia uwajibikaji nchini zinapata urahisi katika kazi yake.
- v. Itaboresha utekelezaji wa Tanzania katika mpango wa Afrika kujitathmini kiutawala bora (APRM).

2.4.6. Kupambana na rushwa na ufisadi:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itatoa elimu kwa umma kuhusu rushwa na namna wananchi wanavyoweza kushiriki kwa pamoja kutokomeza rushwa kubwa (ufisadi) na ndogo.
- ii. Kwa kushirikiana na mataifa ya jirani na rafiki, itaandaa orodha ya makampuni na taasisi zinatoa rushwa kupata miradi, ili kuondoa mianya ya rushwa katika manunuzi hasa ya nje.

- iii. Kudumisha uwazi katika utendaji wote wa Serikali kwa kurekebisha sheria ya watoa taarifa (Whistle blowers act), ili kutoa kinga na ulinzi kwa watakaofanya kazi hii ya kizalendo ya kutoa taarifa.

2.4.7. Kulinda weledi wa ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itaondoa mashaka yeyote ya kisheria kati ya sheria ya Bunge na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya tafsiri ya mamlaka ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabau za Serikali, ili kuimarisha kinga ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na ofisi yake.
- ii. Itamrejesha kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Prof. Mussa Assad ili kumaliza muda wake kwa mujibu wa Katiba.
- iii. Mfuko wa Ukaguzi utakuwa na Bajeti inayotosheleza kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kuifanya iwe na uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa usahihi na ufanisi Zaidi.

2.4.8. Kulinda maadili ya kazi:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo ili kulinda maadili ya kazi;

- i. Itabadilisha kabisa mfumo na utendaji wa Tume ya Maadili ya Umma ili kuipa nguvu na nyenzo za kusimamia kikamilifu maadili ya utumishi wa umma, kwa kuweka utaratibu wa kisheria utakaoelekeza uteuzi wa Viongozi wa Tume hii kufanywa na Tume ya Kijaji, chini ya Jaji Mkuu na kufanyiwa usaili na kuthibitishwa na Bunge/Kamati ya Bunge ili kuhakikisha wanawajibika kwa wananchi na siyo kwa viongozi wachache wanaowateua.
- ii. Itaunda Kamisheni ya maadili ya jeshi la polisi, kusimamia weledi na maslahi ya polisi hasa katika kuhakikisha jeshi la polisi halitumiki kisiasa.
- iii. Itaunda Tume ya kupambana na unyanyasaji wa kijinsia makazini ili kutengeneza mazingira salama ya kazi, hasa kwa wanawake, na kuhakikisha Tanzania inaridhia na kusimamia utekelezaji wa mapatano ya shirika la kazi duniani (ILO,C190) yanayoelekeza kuondoa ukatili sehemu za kazi.

2.4.9. Uhusiano wa Kimataifa

Serikali inayoongozwa na ACT Wazalendo itafanya yafuatayo ili kurejesha heshima ya Tanzania katika Jumuiya ya Kimataifa

- i. Kurejea katika Mkataba wa Mahakama ya Afrika kikamilifu kwa kuondoa barua ya kuzuia Asasi Zisizo za Kiserakali kuanzisha mashtaka dhidi ya Serikali
- ii. Kutoa Uongozi katika Juhudi za kuimarisha Utangamano wa Afrika Mashariki kwa kuhakikisha kuwa hatua zote za utangamano (haswa Umoja wa Fedha Monetary Union) zinafikiwa katika miaka 5 inayokuja Kwa kutekeleza kikamilifu Mkataba wa Afrika Mashariki na Itifaki ya Soko la Pamoja
- iii. Kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha Jumuiya ya SADC inaimarika na kutekeleza ndoto ya SADC kuwa Umoja wa Forodha katika juhudi za kuunganisha soko la Afrika kupitia AfCFTA ambayo Tanzania itasaini na kuridhia Mkataba wake ndani ya siku 100 tangu kuunda Serikali
- iv. Kutekeleza diplomasia ya kiuchumi kwa ukamilifu wake
- v. Kuwa na mahusiano mazuri na mashirika ya Kimataifa Duniani ili kuwezesha Tanzania kufaidika na fursa zinazopatikana katika Fedha za Maendeleo, Uwekezaji Mitaji na Masoko ya Bidhaa za Tanzania. Tanzania itajiunga tena na Open Government Partnership (OGP)
- vi. Kutekeleza Mamlaka ya kikatiba ya Zanzibar katika Mashirika ya Kimataifa ambayo yanashughulika na masuala yasiyo ya Muungano Kwa kuifanya Zanzibar Kuwa Mwanachama, Kwa mfano FIFA, WHO, UNESCO, UNICEF n.k.



3. UFANISI NA UBORA WA HUDUMA ZA JAMII



3.1. Elimu

Serikali ya ACT Wazalendo, itatoa elimu bila malipo (bure) katika shule za awali, msingi, sekondari, vyuo vya ualimu, vyuo vya ufundi (VETA) na vyuo vya utabibu.

3.1.1. Elimu ya Msingi:

Katika kuendana na ongezeko kubwa la idadi ya wanafunzi hasa shule za msingi kutoka wanafunzi wapatao milioni 11 mwaka 2019 mpaka wanafunzi milioni 16 ifikapo mwaka 2025. Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itaongeze vyumba vya madarasa 24,000 kila mwaka ili kutosheleza ongezeko kubwa la watoto mashuleni.
- ii. Itapanua uwezo wa vyuo vya walimu kudahili ili kuzalisha walimu 20,000 kila mwaka ili kukidhi hitaji la ongezeko la wanafunzi.
- iii. Itafanyia mabadiliko makubwa mtaala wa shule ya msingi na sekondari ili kuhakisha elimu ya msingi inamtengenezea kila mwanafunzi msingi mzuri wa maisha yake, mfano, kuwa na masomo mahususi kama kujitegemea, ubunifu na upembuzi, ili kujenga ufahamu na uelewa wa mambo ya msingi katika kukabiliana na kubadilisha mazingira ya jamii zao.
- iv. Itahakikisha vitabu na zana nyingine za kufundishia na kujifunzia vinatolewa bure kwa kila shule za Serikali kwa ubora na wakati sahihi.
- v. Itahakikisha haki na stahiki za walimu ni kipaumbele cha Serikali ya ACT wazalendo, tunaamini, bila walimu wenye maslahi bora, mazingira mazuri ya kuishi na kufanyia kazi, na fursa za kuongeza taalamu na kupanda madaraja kwa wakati, ari ya kufanya kazi hupungua, na hivyo kudumaza utoaji wa elimu.

3.1.2. Elimu ya Sekondari:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itaboresha ufundishaji, ujifunzaji na ubunifu hasa katika masomo ya sayansi na teknolojia. Hii itakuwa ni pamoja na kuhakikisha kila shule ya sekondari Tanzania ina maabara na maktaba.
- ii. Itaajiri wafanyakazi wasio walimu, kama wana maabara, wakitubi, na walezi (matrons/patrons) ili kuhakikisha ubora wa upatikaji wa elimu na ubora wa malezi ya wanafunzi wakiwa shuleni.
- iii. Itajenga Mabweni yenye huduma zote stahiki hasa kwa watoto wa kike kudhibiti utoro, mdondoko na mimba za utotoni.

3.1.3. Elimu ya Ufundi (Technical Education & Vocational Trainings):

Serikali ya ACT Wazalendo, itahakikisha;

- i. Inarudisha hadhi na tija ya vyuo na elimu ya ufundi ili kutoa hamasa kwa Watanzania wengi zaidi kupata elimu ya ufundi.
- ii. Inawekeza katika elimu iliyojikita katika uvumbuzi wenye kuleta suluhu ya changamoto za kila siku za maisha ya mtanzania, wa kawaida. Tumedhamiria kufanya vyuo vya ufundi siyo tu viwe vyuo vya kujifunza kurekebisha vitu mbalimbali na kusoma historia ya uvumbuzi, bali viwe vyuo vinavyojikita katika kuvumbua na kutengeneza (innovation hubs). Tutaweka utaratibu wa kuhakikisha vyuo mbalimbali vinajenga umahiri katika fani tofauti.
- iii. Itahakikisha kuwa Mitaala ya vyuo vya ufundi inabadilishwa ili kutengeneza mitaala inayotoa mafunzo yanayoakisi mahitaji ya soko la dunia,
- iv. Kuwa katika Kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji) kunakuwa na angalau Chuo kimoja cha Mafunzo ya Ufundi (VETA),
- v. Elimu ya Mafunzo ya Ufundi (VETA) inatolewa bila malipo ya ada.
- vi. Inaweka mfumo utakaomuwezesha mhitimu wa chuo cha VETA kuweza kujiendeza zaidi kielimu na kujiunga na mifumo mingine ya elimu.
- vii. Kunakuwa na vyuo vya Ufundi Mchundo (Technical Schools) vyenye uwezo wa kudahili wanafunzi wasiopungua 10,000, angalau katika nusu ya Mikoa ya Tanzania Bara. Ada ya Masomo (Tuition Fee), Fedha za Vitabu (Stationeries), na gharama za Mafunzo kwa Vitendo (Field Studies/Internship) kwa kila mwanafunzi anayedahiliwa katika chuo cha Elimu ya Chuo cha Ufundi Mchundo itagharamiwa na Serikali.

3.1.4. Elimu ya Juu:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itarudisha uhuru wa wanataluma na watafiti katika kuzalisha na kukuza fikra za kimapinduzi.
- ii. Itatoa ruzuku ya sawa na asilimia 40% ya bajeti ya chuo kwa vyuo vikuu kufanya tafiti mbalimbali zitakazotoa dira na miongozo kwenye fani mbalimbali hasa za sayansi ya jamii ili kuwa na Serikali na jamii inayofanya maamuzi ya kitaalamu.

- iii. Itawekeza kwenye mifumo ya kisasa itakayoongeza ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji katika vyuo vikuu, na kuwapunguzia wahidhiri mzigo mkubwa katika kutoa mihadhara.
- iv. Itaajiri wahadhiri wasiopungua 5,000 kwa miaka mitano ili kupunguza uwiano mkubwa uliopo kati ya wahadhiri na wanafunzi.
- v. Itaboresha mazingira mazuri ya vyuo hasa ujenzi wa vyoo na mifumo ya maji safi na majitaka.
- vi. Itadhibiti ubora wa vyuo vikuu binafsi ili kuhakikisha kila chuo kinaandaa wahitimu walio bora na wenye weledi wa hali ya juu.
- vii. Itanzisha vyuo vikuu vya Taifa vipya vitano vyenye uwezo wa kudahili wanafunzi wasiopungua 20,000 kila kimoja, vitatu Tanzania Bara (Mtwara, Kigoma na Tanga), viwili Zanzibar (Pemba na Unguja).
- viii. Itafuta mikopo yote ya miaka ya nyuma iliyotolewa kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu.
- ix. Italipa Ada ya Masomo (Tuition Fee), Fedha za Vitabu (Stationeries), na gharama za Mafunzo kwa Vitendo (Field Studies/Internship) kwa kila mwanafunzi anayedahiliwa kwenye Chuo Kikuu.
- x. Itatunga Sheria kuhakikisha kuwa Mikopo ya Elimu ya juu itakuwa ni kwa ajili ya gharama za kujikimu tu (Meals & Accomodations).
- xi. Itafuta mikopo yote ya wahitimu wote watakaoingia mikataba maalum na Serikali ya kufanya kazi kwa miaka mitatu mfululizo katika maeneo ya pembezoni na yenye mazingira magumu ya kazi, kwa zile sekta mahsusi (Mfano Utabibu na Ualimu, Maafisa Ugani kwa Kilimo, Ufugaji na Uvuvi nk),
- xii. Itarasimisha na kulipia mafunzo kwa vitendo (paid internship), kwa fani zote kwa kipindi kisichopungua miezi sita ili wanafunzi wote wapitie mafunzo kwa vitendo kikamilifu, vilevile kuweka utaratibu wa kutumia matokeo ya mafunzo kwa vitendo katika utoaji ajira ili kuhimiza wanafunzi kuona umuhimu wa mafunzo kwa vitendo.
- xiii. Itaweka vivutio maalum vya kikodi kwa makampuni binafsi yatakayotoa nafasi kwa vijana waliohitimu kufanya mafunzo kwa vitendo.
- xiv. Itahakikisha vyuo vikuu vyote nchini vinaweka sheria kali na taratibu mahususi kuzuia rushwa ya ngono.
- xv. Itahakikisha vyuo vikuu vyote vinakuwa na program maalum inayolenga kutengeneza mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu kupata elimu ya juu katika fani walizochagua kwa urahisi na ufanisi.



3.2. Afya

Serikali ya ACT wazalendo inaamini kwamba, huduma bora za afya ni haki ya msingi ya kila Mtanzania. Serikali ya ACT Wazalendo itawekeza zaidi katika ‘Elimu ya afya’ na ‘Afya ya msingi’ ili kuzuia magonjwa na kuwawezesha Watanzania kupata huduma bora ya afya kupitia Bima ya Afya na kwa kutumia mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Serikali kwa kushirikiana na sekta za Elimu, Maji, Nishati, Mazingira, Usalama barabarani na Kilimo, itahakikisha elimu ya Afya inawafikia Watanzania wote ili wawe na uwezo wa kulinda afya zao na kujiepusha na maradhi yanayoambukiza na yasiyoambukiza, hasa yanayotokana na mfumo wa maisha (life style diseases) na majeraha.

Serikali ya ACT Wazalendo itaunda mfumo wa huduma za afya kwa kuzingatia misingi ya usawa na ushirikishwaji wa jamii katika kufanya maamuzi yanayohusu maswala ya afya, sera bora za huduma za afya, na kuchochea uwajibikaji, ili kupunguza kwa asilimia 30 vifo vya mapema vitokanavyo na magonjwa yasiyoambukiza na kutokomeza magonjwa makuu yakuambukiza kama malaria na kifua kikuu ifikapo mwaka 2030.

Serikali ya ACT Wazalendo itaboresha bajeti ya huduma za afya mwaka hadi mwaka ili kuboresha elimu ya afya, nguvu kazi, upatikanaji wa dawa na vitendea kazi, teknolojia, miundombinu pamoja na mfumo mzima wa kutoa huduma za afya ambao utatumika nchi nzima.

3.2.1. Kuboresha miundombinu ya utolewaji wa huduma za Afya:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itasimamia ujenzi wa zahanati mijini na vijijini kufikia lengo la kuwa na zahanati 1 kwa watu 1000.
- ii. Itajenga na kuboresha hospitali za mikoa na kuzifanya ziwe za kisasa na zenye kukidhi viwango vya kimataifa, ikiwa ni pamoja na kuwekeza na kuboresha huduma za uchunguzi (diagnosis) kwenye kila hospitali ya mkoa.
- iii. Itafanya uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya afya kwa kuwa na hospitali kubwa tatu za kanda zenye hadhi, uwezo na viwango vya kimataifa. Hospitali hizo zitajengwa katika mikoa ya Mara, Ruvuma na Singida.

3.2.2. Wafanyakazi wa sekta ya afya:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itawawezesha Wafanyakazi wa afya hasa kwenye ngazi ya zahanati kutoa elimu ya afya kwa umma wakishirikiana na viongozi wa Serikali za Mitaa, vitongoji na vijiji, ili kuzuia maradhi mbalimbali.

- ii. Itasimamia utaratibu wa wanafunzi wa shahada ya kwanza ya utatibu, kupewa mafunzo ya huduma za afya ya msingi kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo (internship), kabla ya kuhitimu masomo yao.
- iii. Itatenga fedha maalumu za ufadhili kwa masomo ya utabibu na ukunga ili kufikia lengo la kuwa na daktari mmoja kwa kila watu 1000 ifikapo mwaka 2030.

3.2.3. Utoaji wa huduma za afya:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

- i. Itaboresha, kuwekeza na kuwezesha utoaji huduma za 'elimu ya afya', kwa kuanzisha utaratibu wa kuwa na mhadumu/mtaalamu wa afya wa mtaa/Kijiji (bibi/bwana afya). Msisitizo mkubwa utawekwa kwenye 'elimu ya kinga' kabla ya 'tiba'.
- ii. Itahakikisha katika kila nyumba 100 kunakuwa na mtaalamu wa afya (tabibu/Muuguzi), ili kufuatilia mienendo ya afya za Wananchi kwa kuangalia historia za afya ya familia, hali ya mazingira, usafi wa nyumba nk.
- iii. Kuhakikisha wazee, mama wajawazito, watu wenye ulemavu ambao wanahitaji huduma za afya mara kwa mara, pamoja na wanawake, na watoto wahanga wa ukatili watapatiwa matibabu bila malipo.
- iv. Kuhakikisha kila hospitali ya wilaya inakuwa na daktari bingwa wa akina mama na watoto.
- v. Kutoa bure chanjo za magonjwa mbali mbali, hasa kwa ajili ya watoto na zenye kulinda watanania juu ya magonjwa yenye kuambukiza ay a milipuko.

3.2.4. Mfuko wa Bima Afya:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itaboresha mfuko wa Bima ya Afya kwa kuunganisha na mifumo ya Hifadhi ya Jamii, ili kila Mtanzania anapochangia hifadhi ya jamii awe anapata huduma ya Afya moja kwa moja. Kwa mfumo huu, mfuko wa Bima ya Afya utaweza pia kupata fedha kwa wakati na kulipa watoa huduma kwa wakati. Bima ya Afya ni haki ya kila Mtanzania.
- ii. Itaisimamia kikamilifu haki ya kila Mtanzania kuwa na Bima ya Afya yenye kumpa kinga ya matibabu bila kujali hali yake ya kiafya (wakati wa kujiunga na bima).

3.2.5. Mfumo wa taifa wa kukusanya taarifa za afya:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itawekeza kwenye mfumo wa TEHAMA utakaoweza kukusanya na kuhifadhi taarifa za wagonjwa nchi nzima kwa urahisi, ufanisi, uhakika na kwa wakati, hivyo kuwafanya matabibu kuwa na historia sahihi ya mgonjwa,
- ii. Itatumia mfumo huu pia kukusanya mapema taarifa za magonjwa ya mlipuko na kuboresha upatikanaji wa taarifa kwa ajili ya tafiti mbalimbali.

3.2.6. Upatikanaji na usambazaji wa dawa na vifaa vya matibabu:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itawekeza kwenye utafiti na uzalishaji wa dawa salama ndani ya nchi pamoja na vifaa tiba.
- ii. Itaweka utaratibu maalumu wa kuwezesha kimitaji viwanda vya ndani na vyuo vya ufundi ili viweze kuzalisha dawa na vifaa vya tiba kwa kiwango cha kimataifa, ili kukidhi soko la ndani na kushindana katika soko la nje.
- iii. Itaimarisha mfumo wa usambazaji dawa na vifaa tiba kwa kutumia teknolojia mbalimbali za mawasiliano, na kudhibiti ubora wa dawa na vifaa vya afya vinavyotumika nchini.




3.3. Maji

Ili kuhakikisha upatikaji wa maji safi na salama kwa kila Mtanzania, Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itawekeza kiasi cha shilingi Trilioni 10 ndani ya miaka mitano, wastani wa Shilingi Trilioni 2 kwa kila mwaka, kwenye kumaliza kabisa tatizo la maji safi na salama kwa Wananchi. Hii ni pamoja na kujenga na kupanua miundombinu ya maji safi na maji taka.
- ii. Ili kuhakikisha utendaji ulio na ufanisi, Serikali itahakikisha Wizara ya Maji inashirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Afya na TAMISEMI, hasa idara za mipango miji na Serikali za Vijiji ili kuhakikisha miundombinu ya maji safi na maji taka inatandazwa kwa mujibu wa mipango ya matumizi ya ardhi.
- iii. Itaimarisha Mfuko wa Maji kwa kuupa chanzo cha uhakika cha mapato kutoka Ushuru maalumu utakaotokana na matumizi ya mafuta ya Petroli nchini.

- iv. Itatoa ruzuku kwa Mamlaka za maji ili kuziwezesha kupanua na kuboresha miundombinu ya maji katika maeneo yao. Upanuzi wa miundombinu ya maji utazingatia mahitaji, usawa na mipango ya miji/vijiji na si nani anaweza kulipa ankara, shabaha ni kuyafanya maji kuwa huduma ya muhimu na sio biashara.
- v. Itatoa ruzuku ya upatikaji wa maji bure kwa kaya masikini, zinazoendeshwa na wanawake au kaya zinazoishi na watoto wenye ulemavu wanaohitaji uangalizi maalum.
- vi. Itahakikisha Taasisi zote za Serikali zinakuwa mfano kwa kuwa na huduma sahihi na endelevu za utoaji huduma ya maji na uhifadhi wake.
- vii. Itaratibu huduma za maji zinazotolewa na watu binafsi ili kudhibiti usalama wa maji na gharama za huduma hiyo.
- viii. Itawekeza katika kuhamasisha vijana kuvumbua mbinu mbalimbali za kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama, uhifadhi endelevu wa maji safi hasa ya mvua na udhibiti wa maji machafu nchi nzima.



3.4. Nishati endelevu

Tutaongeza uzalishaji wa umeme kutoka megawati 1500 za sasa mpaka megawati 5400. Kati ya hizo megawati 3264 zitatokana na umeme wa maporomoko ya maji, megawati 1500 zitazalishwa kutoka gesi asilia na megawati 636 zitazalishwa kutoka vyanzo mbalimbali vya nishati jadidifu. Katika sekta ya nishati Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itaongeza matumizi ya gesi ya Mtwara kuzalisha Umeme kutoka chini ya 20% hadi 60% kufikia mwaka 2025, kwa kujenga vituo vya kuzalisha umeme katika Mikoa ya Mtwara na Lindi na kuingiza umeme huo kwenye Gridi ya Taifa.
- ii. Itaongeza kiasi cha umeme kinachozalishwa kutoka megawati 1,500 za sasa mpaka megawati 5,400 kufikia mwaka 2025. Kati ya hizo, megawati 1,238 zitatokana na umeme unaozalishwa na maporomoko ya maji (hydroelectric power plants), megawati 1,800 zitazalishwa kutoka Gesi Asilia na megawati 862 zitazalishwa kutokana na vyanzo mbalimbali vya nishati jadidifu ikijumuisha umeme jua, makaa ya mawe, upepo na joto ardhi.
- iii. Itatumia nishati ya umeme jua (solar energy) inayopatikana kwa wingi na bure kila siku baada ya gharama za awali kuhudumia

zahanati, vituo vya afya, shule za msingi na sekondari za Serikali ili kupunguza mzigo kwenye gridi ya taifa, kuondoa gharama za usafirishaji na usambazaji wa umeme kwenye taasisi hizo nchi nzima na kuwa na umeme wa uhakika unaozalishwa kwenye kila taasisi. Itahakikisha Viwanja vyote vya Ndege nchini vinakuwa ni vituo vya kuzalisha Umeme wa Jua ili kuendesha sehemu ya shughuli zao, na ziada kuingizwa kwenye Gridi.

- iv. Itahakikisha Vyama vya Ushirika vya Utumiaji wa Maji Vijijini vinawezeshwa kuendesha miradi yao ya Maji kwa kutumia Umeme wa Jua au Upepo.
- v. Itasambaza bomba la gesi majumbani kwa matumizi ya kupikia ili kupunguza gharama za kutumia umeme, kununua mitungi ya gesi na kuokoa mamilioni ya misitu inayopotea kila mwaka kwa matumizi ya kupikia majumbani.
- vi. Itaendelea kusambaza umeme kwa kasi hasa vijijini, sambamba na kupunguza gharama za umeme. Kuunganisha mikoa na wilaya zote kwenye grid ya taifa.
- vii. Itapunguza gharama za umeme kwenye matumizi ya kijamii, kama gharama za kusukuma maji, ili kupunguza gharama za kulipia maji kwa wananchi.
- viii. Itarejesha Mradi wa Gesi Asilia (LNG Plant) kwa kuharakisha mazungumzo na wawekezaji na kuondoa vikwazo vyote ili kuwezesha nchi yetu kuwa mzalishaji mkubwa wa gesi katika Afrika, kuongeza ajira kutokana na viwanda na huduma na kuongeza mapato ya fedha za kigeni kutokana na mauzo nje ya Gesi Asilia.



3.5. Hifadhi ya Jamii

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itawezesha kila Mtanzania kujiunga na mfumo wa hifadhi ya jamii. Mifuko ya hifadhi ya jamii itaunganishwa moja kwa moja na huduma za afya na bima ya majanga ili kupunguza msururu wa michango/mifumo hasa kwa Watanzania walio katika sekta binafsi na kwa waajiri.
- ii. Itapunguza michango kwenye hifadhi ya jamii kutoka asilimia ishirini (20%) ya sasa mpaka asilimia kumi na mbili (12%), kwa mchanganuo wa asilimia tisa (9%) kuwa mchango wa akiba ya hifadhi ya jamii, asilimia mbili (2%) kuwa mchango wa Bima ya Afya, na asilimia moja (1%) kuwa mchango wa mfuko wa fidia kwa wafanyakazi (WCF),

- iii. Itashirikiana na na wataalamu wa huduma za fedha ili kutengeneza mfumo wa bima ya majanga utakaowalinda wananchi hasa wa hali ya chini, wafanyabishara wadogo na wakulima dhidi ya majanga yanayotokana na milipuko ya magonjwa, mafuriko, matetemeko, moto, n.k.
- iv. Italeta fao la bei kwa mazao ya kilimo kwa wakulima wote watakaokuwa wanachama wa mpango wa Hifadhi ya Jamii.
- v. Itatumia Mpango wa Hifadhi ya Jamii kwa wakulima kuendesha miradi mikubwa ya kimkakati ya kuleta mapinduzi ya Kilimo nchini, hasa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, maghala ya uhifadhi na viwanda vya usindikaji.
- vi. Itaanzisha taasisi maalum inayojitegemea itakayojikita katika kutathmini, kuratibu na kudhibiti majanga.



3.6. Makazi Bora

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itawekeza kwenye teknolojia itakayosaidia ufanisi wa kupanga miji. Ndani ya miaka mitano, Serikali yetu itakamilisha upimaji wa miji nchi nzima ili kuhakikisha wananchi wanaishi kwenye maeneo yaliyopimwa na yenye huduma muhimu za jamii.
- ii. Itaanzisha ushirika wa makazi (housing cooperatives), utakaojikita katika kuboresha makazi hasa ya wakulima na wafanyabiashara wandogo mijini na vijijini. Mpango wa Hifadhi ya Jamii kwa wakulima itatumika kikamilifu katika uwekezaji kwenye makazi bora.
- iii. Itaweka utaratibu, kushirikiana na sekta binafsi, hasa taasisi za kifedha, kuwezesha vikundi/ushirika wa vijana mafundi wa nyumba/makazi ili kukuza na kuboresha ufanisi wa sekta ya ujenzi wa makazi nafuu.
- iv. Itaanzisha utaratibu maalumu wa kuboresha makazi holela hasa kwenye maeneo ya miji (slums), na kufanya kila Mtanzania kuishi kwenye makazi yaliyo salama, ya kiutu, yanayofikika na yenye huduma zote muhimu za jamii.
- v. Itaratibu sekta ya upangishaji na ununuzi wa nyumba ili iweze kunufaisha Watanzania wote hasa wa hali ya chini.



4. UCHUMI WA WATU

Ili nchi iwe na uchumi imara na endelevu ni lazima wananchi wake wamiliki uchumi kupitia biashara, kilimo, huduma, uvuvi, ufugaji, utalii n.k. Mapato ya Serikali yanakuwa makubwa na endelevu pale wanachi wanapomiliki shughuli nyingi za uzalishaji na huduma. Kwa njia hii, Serikali inakua na uhakika wa mapato kupitia kodi mbalimbali.

Dhamira yetu ni kujenga Tanzania yenye uchumi wenye manufaa kwa wananchi na Serikali kwa ujumla; na siyo kukuza uchumi wa Serikali pekee au kusherehekea ukuaji wa takwimu za kiuchumi na ongezeko la mapato ya kikodi huku walipakodi (wananchi) wakiachwa katika ufukara, kukata tamaa, hali ngumu za maisha na mazingira magumu ya kutengeneza kipato. Katika kuhakikisha kwamba uchumi wa watu unaimarika na Serikali inapata mapato yake kutokana na uchumi imara wa watu, Serikali ya ACT Wazalendo itajikita katika sekta zifuatazo;



4.1. Biashara zenye Tija na endelevu

Ili kupanua na kujenga biashara shindani, zenye tija na endelevu katika mfumo rasmi na mfumo usio rasmi katika sekta ya biashara, Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itawapa wananchi uhuru na kuondoa urasimu katika kuanzisha na kuendesha biashara yoyote ikiwa ni pamoja na uhuru wa kununua na kuuza bidhaa zozote halali ndani na nje ya nchi bila vikwazo vyovyote.
- ii. Itazitambua na kurasimisha biashara zilizo nje ya mfumo rasmi ili kuzipa uwezo na fursa ya kupata mitaji, teknolojia na masoko.
- iii. Itatambua na kuweka mazingira mazuri ya kisera ili kuendesha biashara kwa njia ya mitandao (e-commerce/digital economy) kwa mafanikio makubwa hasa kwa Watanzania.
- iv. Itaunda mfuko maalumu wa kutoa udhamini, ufadhili na mikopo kwa biashara zinazochipukia (start-ups) zenye ubunifu, hasa ambazo zimejikita katika matumizi ya teknolojia na zinazomilikiwa na vijana na wanawake.
- v. Itawalinda wafanyabiashara na wazalishaji wa ndani na kuwajengea mazingira ya kushirikiana na/au kushindana na wafanyabiashara na bidhaa kutoka nje ya nchi.
- vi. Itatumia diplomasia na mahusiano ya kimkakati na nchi nyingine ili kupanua soko/biashara ya nje kwa mazao na bidhaa nyingine zinazozalishwa hapa nchini. Ili kufikia adhama hiyo, Serikali itatumia ofisi zake za kibalazi duniani kote kuhakikisha Watanzania hasa vijana na wanawake wanashiriki kikamilifu na kwa wingi katika Maonyesho

mbalimbali ya biashara na sanaa ya kimataifa. Pia ofisi za balozi zitakuwa chachu katika kutafuta na kuwezesha upatikanaji wa fursa za kibiashara na washirika wa kibiashara nje ya nchi, ili kuimarisha urari wa kibiashara (balance of trade), kuongeza fedha za kigeni hapa nchini na kuitangaza Tanzania kama mzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

- vii. Itahamasisha na kuwawezesha wawekezaji wa ndani katika sekta ya viwanda, uzalishaji na umiliki wa miundombinu kama vile umeme, maji, ndege, nishati ya gesi, vivuko n.k., kupitia mfumo wa Ubia wa Sekta binafsi na Sekta ya Umma, yaani PPP (Public, Private Partnerships),
- viii. Itawauzia Watanzania mpaka asilimia 51 za hisa za makampuni makubwa yanayomilikwa na Serikali kwa sasa ili wananchi washiriki moja kwa moja kumiliki uchumi wao na kuongeza ufanisi na uwazi wa mashirika hayo kupitia masoko ya mitaji.
- ix. Itapitia mifumo yote ya kodi na kuhakisha kunakuwa na kodi rafiki kwa wananchi. Kodi sahihi zinazotowwa kwa wakati sahihi ili kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiyari, na muhimu zaidi ili kuhakisha biashara zinakua na kuimarika na siyo kuwa na mfumo wa kodi ambao utapelekea kufunga au kuua biashara. Halikadhalika, Serikali ya ACT Wazalendo itaondoa mfumo unaomlazimisha mfanyabiashara kulipa kodi kabla hajaanza kufanya biashara.



4.2. Ajira

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itatengeneza ajira zenye tija milioni kumi (10) ndani ya miaka mitano. Ajira million tano (5) kutoka kwenye mnyororo wa thamani wa sekta ya kilimo, ajira million 2 kutoka sekta rasmi na ajira milioni 3 kutoka sekta isiyo rasmi.
- ii. Itaimarisha ubora na kutafuta soko la nje kwa kazi za ubunifu kama uhunzi, uchongaji, uchoraji na bidhaa zingine zitokanazo na kazi za mikono.
- iii. Itaweka mifumo mizuri ya kisera na uwekezaji katika soko la sanaa na michezo, Serikali yetu kupitia wizara husika itafanya uwekezaji wa kina kwenye kuimarisha, kuinua na kutengeneza ajira zenye tija zisizopungua laki tano kwenye soko la sanaa na buruduni na mnyororo wake wa thamani.
- iv. Itaboresha maslahi ya wafanyakazi wa sekta ya umma na kusimamia maslahi stahiki ya wafanyakazi wa sekta binafsi ili ajira zote zitakazozalishwa kipindi cha uongozi wetu ziwe ajira zenye tija na zenye kukidhi mahitaji ya wafanyakazi na kupatiwa hifadhi ya jamii stahiki.

- v. Itapunguza kodi ya wafanyakazi (PAYE), lengo likiwa kuwaongezea wafanyakazi kipato ili waweze kumudu mahitaji katika maisha, kujiwekea akiba au kuanzisha na kuendesha shughuli za uzalishaji kipato cha ziada.
- vi. Itatengeneza mazingira mazuri ya kisera yatakayowezesha vyama vya wafanyakazi kuwa huru, kuimarika na kusimamia maslahi ya wafanyakazi kwa ufanisi.
- vii. Kulipa mafao ya watumishi kwa wakati na kuboresha maslahi na huduma kwa wastaafu.



4.3. Michezo, Sanaa na Burudani

Tanzania imejaaliwa vibaji na vipawa vya hali ya juu katika nyanja ya sanaa na michezo. Ili kufufua utajiri uliojificha kwenye sekta hiyo, Serikali yetu itafanya yafuatayo

- i. Kurudisha Serikalini maeneo ya wazi yaliyoporwa, na kutenga maeneo mapya ya wazi kwa ajili ya michezo na mapumziko. Serikali yetu itaingia ubia na vikundi vya wanawake na vijana katika kuhakikisha maeneo ya wazi yanatumika kwa ajili ya burudani, starehe pamoja na kutengeneza ajira kwa vijana.
- ii. Kuunda Mamlaka ya Viwanja vya Michezo ili kujenga, kuendeleza na kutunza Viwanja vya michezo kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi.
- iii. Kutengeneza Sera ya Mambo ya Nje ambayo, michezo na burudani ni moja kipaumbele cha mashirikiano yetu na nchi nyingine.
- iv. Kujenga kumbi tano kubwa za matamasha (Arena) Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma ili kuhakikisha sanaa inapewa hadhi na thamani yake na Watanzania wanakula bata kwenye mazingira mazuri.
- v. Kushirikiana na vyama vya waandishi wa vitabu Tanzania, ili kutengeneza mfumo bora wa kuwekeza kwenye sekta ya uandishi ili kufanya uandishi kuwa ajira yenye tija, na kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza kwenye mnyororo wa thamani wa uandishi, hasa usambazaji, kwa lengo la kutengeneza taifa lenye hamasa ya kusoma na kuhifadhi maarifa kupitia uandishi wa vitabu (uandishi).
- vi. Kutoa ruzuku ya Kikodi kwa Kampuni Binafsi au watu binafsi wanaowekeza kwenye sekta ya michezo. Kwa mfano Kampuni binafsi

yenye timu za michezo, kama mpira wa miguu, mpira wa meza, mpira wa mikono nk. kuruhusiwa kuondoa gharama za uendesaji wa Timu katika kukokotoa kodi ya Mapato (Sports Development expenses to be tax deductible in calculating taxes payable by private companies)

- vii. Kuwezesha uwekezaji kwenye shule za michezo (Sports Academies) kwenye Kanda zote 8 za nchi yetu ikiwemo kuhamasisha mashirika ya umma kuanzisha, kumiliki na kuendesha timu za michezo mbalimbali pamoja na Shule za Michezo ili kukuza michezo nchini na kukuza vipaji vya Vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.



4.4. Kilimo, mifugo na uvuvi

ACT Wazalendo inatambua kwamba, mazao yote ya chakula ni mazao ya biashara kutokana umuhimu na uhitaji mkubwa wa mazao hayo kwa matumizi ya binadamu, mifugo, nishati na viwanda, ndani na nje ya nchi. Katika kuhakikisha kwamba tunapata mapinduzi makubwa ya sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi nchini, Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itatenga 20% ya bajeti ya maendeleo kwenye Sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi, mara mbili zaidi ya makubaliano yaliyozimiwa na Umoja wa Afrika(CAADAP).
- ii. Itapanua na kuboresha vyuo vya kilimo, na kuwekeza kiasi kisichopungua shilingi bilioni 100 kwa mwaka katika utafiti, usambazaji wa mbegu bora za kilimo na kutengeneza mnyororo wa thamani kwa kila zao linalozalishwa hapa nchini.
- iii. Itafungamanisha sekta ya kilimo na sekta ya viwanda, kwa kuhakikisha kwamba viwanda vya ndani vinapata zaidi ya asilimia 80 ya mahitaji yao kutoka kwa wakulima, na kwamba wakulima wanafaidi bei nzuri ya mazao yao na soko la uhakika.
- iv. Itatengeneza mahusiano ya karibu ya kikazi kati ya vyuo vya ufundi, vyuo vya kilimo, vyuo vya masoko na biashara na vyuo vya jamii ili kuhakikisha utaalamu, taaluma na uvumbuzi unachagiza ukuaji wa sekta ya kilimo, uvuvi na mifugo na kutengeneza ajira zenye tija zisizopungua milioni 5 kwenye mnyororo wa thamani ndani ya miaka 5.
- v. Itaunda 'Mamlaka ya Kilimo' ili kusimamia sekta ya kilimo. Wajibu wa mamlaka hiyo ni kuhakikisha mazao yote ya kilimo ya wananchi yamenunuliwa kwa bei nzuri na kuboresha ufanisi katika usambazaji wa pembejeo za kilimo. Mamlaka hii itafanya kazi kwa karibu na vyuo vya ufundi, vituo vya utafiti wa kilimo na viwanda vya ndani kuhakikisha zaidi ya 60% ya pembejeo za kilimo zinazalishwa ndani ya Tanzania.

- vi. Itabainisha aina ya mazao ya kimkakati kwa kila mkoa/kanda na kuhamasisha uzalishwaji wake kwa wingi, ikiwa ni pamoja na kuweka mpango mzuri wa kuongeza thamani ya mazao hayo kabla ya kuyauza kwenye masoko ya ndani na nje.
- vii. Itaruhusu wakulima, wavuvi na wafugaji kuuza mazao yao popote watakapo ndani na nje ya nchi bila vikwazo au masharti magumu.
- viii. Itaanzisha mfuko maalumu wa kilimo kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa miradi ya kimkakati ya kilimo, hasa miradi ya uanzishwaji wa viwanda vya kusindika na kusambaza mazao ya wakulima.
- ix. Itapanua huduma za Benki ya Kilimo kila mkoa. Tutaimarisha na kuiongezea uwezo ili iweze kutoa mikopo yenye riba ndogo na inayolipwa kulingana na msimu wa kilimo.
- x. Itatoa msukumo wa pekee kwa mazao ya michikichi, alizeti na miwa, ikiwa ni pamoja na kuchochea uanzishaji wa viwanda vingi vya kuzalisha mafuta ya kula na sukari ili ndani ya miaka 5 tuache kabisa kuagiza mafuta na sukari kutoka nje ya nchi.
- xi. Itaongeze idadi ya maafisa ugani na kuwaendeleza kitaaluma na kuwapa nyezo muhimu za kufanyia kazi, ili waweze kuwafikia na kuwaelekeza wakulima na wafugaji mbinu bora za kilimo chenye tija ili kuongeza uzalishaji na kipato cha mkulima na mfugaji.
- xii. Itawekeza katika miundombinu ya umwagiliaji inayolinda na kuhifadhi mazingira. Tanzania ina hazina ya hekta milioni 29 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Msukumo mkubwa utawekwa kwenye umwagiliaji endelevu kwa kutumia nishati ya jua (solar irrigation schemes), ili kuwaendeleza wakulima wadogo na wakati kutumia maji yaliyo chini ya ardhi. Tutapanua kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta laki 5 zinazolimwa sasa mpaka hekta million 1.5 ifikapo mwaka 2025.
- xiii. Itawekeza katika uhifadhi, uzalishaji na usambazaji wa mbegu asilia, ama ziwe za jadi au zilizoboreshwa na kukomesha matumizi ya mbegu zilizobadilishwa vinasaba maabara (genetically modified seeds).
- xiv. Itatoa msukumo mpya kwenye kilimo hai (organic farming), ili kuongeza uzalishaji wake na kukidhi soko kubwa lililopo nje ya nchi. Utafiti unaonesha ongezeko kubwa la mahitaji ya bidhaa zinazozalishwa kwa kutumia mfumo huu wa kilimo, hali hii inatoa uhakika wa kutengeneza ajira yenye tija kwenye kilimo cha aina hii. Muhimu zaidi, kilimo hiki kinasaidia sana katika kutunza na kuhifadhi mazingira. Serikali kwa kushirikiana na taasisi za kimataifa, itaboresha mfumo wa uthibitishaji wa mazao yatokanayo na kilimo hai. Maafisa

ugani, vyama vya wakulima na watendaji wa Serikali watajengewa uwezo ili kuhamasishwa na kuwezesha wa kulima kulima kwa kutumia mfumo wa kilimo hai.

- xv. Itatoa kipaumbele maalumu kwenye kilimo cha mbogamboga (organic) na matunda, hasa kwa uwezo wake wa kuingiza fedha za kigeni kutokana na ukubwa wa soko la kigeni, lakini pia ni kilimo kinachofanywa zaidi na wanawake na vijana, hivyo kutengeneza ajira kwa makundi hayo, lakini muhimu zaidi ni kilimo kitakachoboresha hali ya lishe hasa kwa watoto na akina mama wajawazito na kupunguza magonjwa ya utapia mlo, udumavu na maradhi mengine yanayoletwa na mfumo wa maisha.
- xvi. Itajenga maghala kwa ajili ya kuhifadhi nafaka, na majokofu (cold rooms) kwa ajili ya kuhifadhi mbogamboga na matunda, katika kila wilaya ya Tanzania bara na mikoa yote Tanzania visiwani.
- xvii. Katika kutambua mchango wa uvuvi na ufugaji, itawekeza na kuhakikisha uvuvi na ufugaji endelevu unafanyika kote nchini, ikiwemo kuwekeza katika minada ya kisasa na kupanua soko la bidhaa za ufugaji na uvuvi ndani na nje ya nchi. Serikali pia itaboresha mazingira ya kufanya biashara kwa mazao ya majini kama mwani, ili kuwanufaisha wavuvi nchini.
- xviii. Itatenga maeneo maalumu kwa wafugaji, na kuwekeza katika miundombinu ya maji na malisho ili kumaliza migogoro kati ya wakulima na wafugaji.
- xix. Itahakikisha kwamba miundombinu ya huduma za maji, barabara, mawasiliano, masoko, huduma bima na mikopo zinawafikia ili kuwawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi kufanya shughuli zao kwa urahisi na kuwa na hakika ya mapato yatokanayo na kazi zao. Lengo ni kuwafanya waishi maisha yenye uhakika; maisha yenye raha na furaha.



4.5. Kujenga Utajiri wa Jamii kupitia Ushirika wa kisasa

Kuongezeka kwa tofauti za kipato ni changamoto inayoikumba dunia na Tanzania, kwa upande mmoja matajiri wanazidi kunufaika na mifumo ya kiuchumi iliyopo na upande mwingine ukosefu wa ajira kunazidi kushika kasi. Hii inaamsha ari ya kufikiri njia mpya za kuleta usawa wa kimapato. Njia mojawapo ya kupata suluhu ya matatizo haya ni kwenda kwenye chanzo -- kurekebisha mfumo wa uzalishaji, ukusanyaji kodi na mgawanyo wa utajiri ya Taifa.

Kwa mantiki hio, ni muhimu kutumia mfumo wa kujenga uchumi unaohusisha jamii nzima, ambapo wananchi wanaweza kushiriki katika umiliki wa mali na uchumi wao kupitia vyama vya ushirika, jumuiya za wananchi au Serikali za Mitaa. Chama cha ACT Wazalendo kimeanzisha Azimio la Tabora lenye lengo hilo; kuchochea wananchi kushika hatamu za uchumi na kumiliki nyenzo kuu za uzajishaji. Vyama vya Ushirika vya Wananchi vitawezesha wananchi kumiliki njia za uzalishaji, mitaji, usambazaji, masoko na faida.

Kufikia mwaka 2018 kulikua na Vyama Ushirika 10,990 vyenye wanachama milioni 2.5 (sawa na 5% ya wataanzania). Vyama hivi hasa SACCOs vinasaidia sana wanachama wao kupata mikopo midogo ya biashara, kusuluhisha matatizo ya dharura na kijamii n.k. ACT Wazalendo itaimarisha zaidi Ushirika ili kuwezesha wananchi kumiliki uchumi wao kwa njia zifuatatazo;

- i. Itaweka mazingira ya kisera na kuwekeza katika ushirika utakaomilikiwa na wanaushirika kwa ajili ya maendeleo yao. Ushirika wa wakulima, wafugaji na wavuvi utakakuwa ni nyenzo ya wanaushirika kujiunga na hifadhi ya jamii, kupata bima ya afya, makazi yenye hadhi na staha, kuwekeza kwa pamoja, kusimamia bei na mauzo ya mazao yao nakadhalika.
- ii. Itawezesha kisera na kisheria kuunganishwa kwa wakulima, wavuvi na wafugaji na masoko makubwa ya nje ya nchi kupitia vyama vyao vya ushirika na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo. Zaidi, tutahakikisha kunakuwa na ushindani baina ya wafanyabiashara ili wakulima wapate bei nzuri kwa mazao yao.
- iii. Itaondoa unyonyaji unaofanywa na madalali (middlemen) kwenye soko la mazao, kwa kuimarisha mfumo wa taarifa ya masoko ya mazao, kwa kutumia mifumo ya TEHAMA itakayowezesha wakulima kuuza mazao yao moja kwa moja kwa mtumiaji kwa njia ya mtandao. Serikali pia itahusika kikamilifu kwenye hifadhi ya mazao na kuanzisha mfumo wa soko la bidhaa (commodities exchange), ambao utashirikisha wakulima wenyewe kupitia vyama vyao vya ushirika.
- iv. Pale ambapo madalali ni lazima kwa sababu za kihistoria, kiuchumi na kimazingira, Serikali itahalalisha udalali wa asili kwa kuurasimisha.



4.6. Ardhi kwa maendeleo ya Watanzania

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya mapinduzi makubwa katika msingi, mfumo na muundo wa umiliki wa ardhi, kwa kuwa inatambua na kuamini kuwa ardhi haipaswi kuwa bidhaa au mtaji wa wachache kuzalisha faida/kulimbikiza mali. Tunataka kufanya ardhi kuwa mtaji kwa mamilioni ya Watanzania hasa vijana na wanawake. Ili kuhakikisha umilikaji ardhi unajikita katika misingi ya haki, usawa na utu. Ili kuyafikia hayo Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itaanzisha mfumo mpya unaozingatia demokrasia na ushirikishwaji wa wananchi kutoka katika ngazi za utumiaji, umiliki na usimamizi/udhibiti wa ardhi kupitia vyombo vya uwakilishi vilivyo karibu na wananchi.
- ii. Itaweka utaratibu wa kuzijengea uwezo halmashauri za vijiji, kamati za ardhi za vijiji na mabaraza ya ardhi ya vijiji katika kusimamia ardhi na utajiri wote uliopo ndani ya mipaka ya vijiji kwa niaba ya umma wa vijiji husika.
- iii. Itaweka utaratibu maalumu wa kuhamasisha na kurahisisha umilikaji ardhi kwa vijana na wanawake - na siyo kusubiri mirathi au kulanguuliwa kwenye soko. Hii ni pamoja na kuhakikisha wanawake na vijana wanashiriki kikamilifu katika maamuzi na kunufaika na mazao (fidia au faida) yanayotokana na rasilimali-ardhi ya familia.
- iv. Itazilinda kisheria na kuzipa hadhi sawa haki za umiliki wa ardhi ya kimila kama ilivyo kwa hati zinazotolewa na Serikali kuu.
- v. Itaondoa utaratibu wa kutoza kodi za ardhi kwa ardhi za kijiji, kutokana na ukweli kwamba dhana ya umiliki kati ya wanakijiji hutofautiana na ile ya wawekezaji ambao hutumia ardhi kwa ajili ya kuzalisha faida au kulimbikiza mali wakati wananchi, wakulima wadogo hutumia kujikimu na kujihifadhi.
- vi. Itafuta gharama za upimaji wa viwanja nchi nzima, kupanga miji ni utakuwa wajibu wa Serikali yetu.
- vii. Itaunda Tume ya taifa ya uchunguzi (na kufanyia kazi papo hapo mapendekezo yatakayotolewa), wa athari walizozipata na wanazozipata wananchi juu ya uporaji, uvamizi na unyang'anyi unaotokana na sera na sheria mbovu za ardhi zinazotekelezwa na Serikali zilizopita zinazokumbatia soko huria lisilojali maslahi ya wananchi wanyonge.
- viii. Itarejesha na/au kugawa upya ardhi kwa Wananchi walioporwa na walionyang'anywa kupitia ubinafsishwaji kutoka kwa mashiriki ya Umma na makampuni hodhi.


- ix. Ili kuondoa ukiritimba wa umilikaji wa ardhi, itaunda baraza la Ardhi la Taifa kama chombo huru kitakachokuwa na miliki ya hati ya ardhi ya jumla (general lands) na ardhi ya hifadhi, ambalo litawajibika kwa chombo chenye uwakilishi wa wananchi kitaifa (bunge). Na kuweka ardhi ya kijiji kwenye mikono ya wananchi wenyewe kupitia vyombo vyao vya maamuzi.



4.7. Kujenga Miundombinu Wezeshi

Ili kuifikia Tanzania inayokua kiuchumi na yenye raha na furaha, kujenga na kuwekeza katika miundombinu mbalimbali ni kipambaule cha Serikali ya ACT Wazalendo. Tunaamini miundombinu bora, yenye kufikia wengi na kurahisisha ufanyaji kazi na ufanisi ni nguzo ya uchumi wa watu. Kwetu sisi ACT Wazalendo, miundombinu ni nyenzo tu ya kufikia maendeleo, hivyo, Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itaendeleza juhudi za kufufua reli ya kati na kuunganisha mikoa kwenye mfumo madhubuti wa reli utakaorahisisha usafirishaji wa bidhaa kwa urahisi ndani na nje ya nchi.
- ii. Itajenga reli ya kuunganisha mradi wa Mchuchuma na Liganga na Bandari ya Mtwara ili kusafirisha madini ya chuma, bidhaa za chuma, makaa ya mawe na bidhaa nyengine zinazotokana na mradi huo.
- iii. Itajenga reli ya kuunganisha mradi wa Kabanga Nickel na reli ya kati ili kusafirisha madini ya Nickel kupitia bandari za Dar na Bagamoyo.
- iv. Itajenga mifumo imara ya barabara hasa kutoka kwenye vijiji na mashamba ya ushirika ya wakulima wadogowadogo na kuunganisha na barabara kuu.
- v. Itajenga barabara kwenye maeneo yanayozalisha mazao makuu yanayoliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni. Katika miaka mitano inayokuja tutajenga barabara ya korosho kwa kutumia fedha zinazotokana na ushuru wa korosho (Export Levy).
- vi. Itajenga masoko ya kisasa kila wilaya, na kuhakikisha masoko yote makubwa na madogo, yana mifumo sahihi ya ukusanyaji na uteketezaji taka, maji safi, mifumo ya maji taka, mahali stahiki kwa uhifadhi wa bidhaa mbalimbali na vyoo vya kutosha.
- vii. Itahakikisha vyoo vya umma vinajengwa katika kila maeneo ya wazi yenye mikusanyiko ya watu nchi nzima.



4.8. Viwanda vya zana na usindikaji

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- i. Itawezesha uwekezaji kwenye viwanda vinavyozalisha vifaa mbalimbali vya viwandani au bidhaa/machine zinazotumika kutengenezea bidhaa nyingine kwa kuweka vivutio stahiki.
- ii. Itawezesha uwekezaji kwenye viwanda vya teknolojia na maabara za kisasa kwa kushirikiana na taasisi za ndani na makampuni ya kimataifa. Utajiri wa karne ya 21 unategemea sana uvumbuzi na matuminzi ya teknolojia. Tumejipanga kuhakikisha kuwa hatutaendelea kuwa soko la teknolojia inayozalishwa na nchi nyingine, bali na sisi tunakuwa wazalishaji wa teknolojia mbalimbali hasa teknolojia za kukabiliana na changamoto zetu watanzania na wa Afrika. Viwanda hivi kwa teknolojia vinatarajiwa kuajiri vijana wasiopungua laki tano kwenye mnyororo wake wa thamani.
- iii. Itawezesha ufufuaji wa viwanda vya kuchakata pamba na kuzalisha nguo (textile industry) ili kuzalisha bidhaa kama vitenge, vijora, madera na batiki zenye ubora wa hali ya juu.
- iv. Itaboresha vivutio ili kuwezesha ujenzi wa viwanda vidogo maeneo ya vijijini vinavyoendeshwa, kumilikiwa na kusimamiwa na wakulima wenyewe kupitia vyama vyao vyao vya ushirika, ambavyo vitaweza kuzalisha ajira na kuchakata mazao.
- v. Itawezesha uwekezaji kwenye viwanda vya kusindika matunda, nyama, samaki na mbogamboga na kuongeza thamani badala ya kuuza mazao kama yalivyotoka shambani.



4.9. Utajiri kwenye maliasili

Tanzania imebahatika kuwa na maliasili nyingi ambazo ni utajiri mkubwa ikiwa zitatumika vyema. Nchi yetu ina hazina kubwa katika utalii, misitu, madini na gesi. Pia bahari, maziwa na mito ni sehemu ya utajiri mkubwa wa Tanzania.

4.9.1. Utalii

Sekta ya Utalii ina uwezo mkubwa wa kuzalisha ajira nyingi nchini iwapo itawekwa vivutio vya kutosha na usimamizi shirikishi kati ya sekta binafsi na Serikali. Uwekezaji mkubwa unatakiwa katika kufungua na kutangaza vivutio vingi zaidi vya utalii katika maeneo mengi ya nchi.

Japokuwa Serikali mpya itakayoundwa baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 itarithi sekta ya Utalii ambayo imevurugwa vya kutosha na janga la COVID 19 (Virusi vya Corona), Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

- i. Itarekebisha sera za kodi ili kuirejesha katika hali yake ya kawaida sekta ya Utalii pamoja na mnyororo wake ambayo imeathirika sana na janga la COVID 19. Marekebisho hayo yatahusisha kutoa ruzuku kwa Kampuni za Utalii na kulinda Ajira za Wafanyakazi wa Sekta ya Utalii.
- ii. Itawekeza kwenye Ujenzi wa miundombinu ya Maeneo ya Utalii ili kufungua vivutio vipya na kuvifanya kufikika kwa urahisi na kwa usalama.
- iii. Itawezesha Sekta Binafsi kuongeza vyumba vya mahoteli kwenye vivutio vya Utalii,
- iv. Itaanzisha kampeni Maalumu ya kufikisha Idadi ya Watalii Milioni 5 watakaolingia nchini ifikapo Mwaka 2025.
- v. Itatumia sekta ndogo za Michezo na Burudani kimkakati kama nyenzo za kukuza Utalii nchini.

4.9.2. Bahari na Bandari:

Serikali ya ACT Wazalendo itatumia nafasi ya Tanzania kijiografia, ya kuzungukwa na nchi nyingi zisizo na bahari, kufaidika kiuchumi na kuhudumia nchi nyingine, shabaha kuu ni kuifanya Tanzania kuwa kituo kikuu cha usafirishaji wa majini (Maritime Hub) katika bara la Afrika na kituo kikuu cha biashara (Trade & Logistics Hub) katika eneo la maziwa makuu. Zaidi, Serikali itatengeneza na kutekeleza sera sahihi zitakazohakikisha Watanzania wananufaika kwa kufanya biashara na nchi zote zinazotuzunguuka kwa kuondoa urasimu katika kupeleka bidhaa nje ili kuongeza mapato yao na fedha za kigeni.

Katika kufikia shabaha hii, Serikali ya ACT Wazalendo itahakikisha yafuatayo:

- i. Kufufua na kuendeleza uwekezaji wa eneo la kiuchumi la Bagamoyo.
- ii. Kuimarisha Bandari ya Mtwara ili kuhudumia korido ya maendeleo ya Mtwara (Mtwara Corridor), ambayo inahusisha mradi wa Mchuchuma na Liganga na Usafirishaji wa Bidhaa kutoka na kwenda katika nchi ya Malawi na kaskazini mwa nchi ya Msumbiji. Vilevile, kuufanya Mji wa Mtwara kuwa kituo cha huduma kwa miradi ya uwekezaji wa mafuta na gesi, kusini mwa Tanzania na Kaskazini mwa Msumbiji.
- iii. Kuimarisha Bandari ya Tanga, kwa kukamilisha uwekezaji wa Bandari ya Mwambani.

- iv. Kuimarisha Bandari ya Kigoma ili kuweza kuhudumia mizigo inayotoka na kwenda mashariki ya Kongo pamoja na nchi ya Burundi.
- v. Kuwezesha uwekezaji kwenye bandari za uvuvi ili kuimarisha uvuvi bahari kuu kufikia lengo la mauzo nje ya mapato ya uvuvi yenye thamani ya dola za kimarekani bilioni 1.

4.9.3. Madini:

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya mapinduzi makubwa katika mfumo wa umiliki na uendeshaji wa miradi katika sekta ya uchimbaji wa madini ili kuhakikisha wananchi wanafaidika na rasilimali ya madini. Shabaha yetu itakuwa ni kufungamanisha sekta ya madini na sekta nyengine za uchumi wa watu, na kuongeza kwa wingi mapato ya fedha za kigeni kutoka dola bilioni 2.5 za sasa mpaka dola bilioni 6 mwaka 2025. Ili kutekeleza hilo, Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

- i. Itabadili mfumo wa umiliki ili uwekezaji kwenye madini kuwa ni kwa utaratibu wa kugawana mapato (Production Sharing Agreement) kati ya mmiliki na mwendeshaji (Contractor).
- ii. Itaweka kisheria utaratibu wa wananchi wanaoishi kwenye maeneo yenye madini kutoa idhini ya mradi wa uchimbaji madini kabla ya kuanza kutekelezwa (Free Prior Informed Consent).
- iii. Itaweka mkazo kwenye miradi ya uchimbaji madini ambayo ina faida kubwa ya fungamanisho, miradi mikubwa miwili ya kipaumbele itakuwa ni Mradi wa Mchuchuma na Liganga wilayani Ludewa, mkoani Njombe, na mradi wa Kabanga Nickel wilayani Ngara, mkoani Kagera.



4.10. Miradi ya Kimkakati

Serikali ya ACT Wazalendo itatekeleza miradi ifuatayo ya kimkakati;

- i. Itasimamia kukamilika kwa uwekezaji wa mradi wa Mchuchuma na Liganga kuzalisha bidhaa za chuma, madini ya vanadium na madini mengine, umeme wa makaa ya mawe na kuongeza mapato ya fedha za kigeni.
- ii. Itasimamia Ujenzi wa mabwawa makubwa 5 ya kuzuia mafuriko na kujenga skimu kubwa za umwagiliaji zenye jumla ya hekta 1,000,000.
- iii. Itatekeleza Ujenzi wa miradi ya maji nchi nzima kuhakikisha kila mtanzania anapata maji safi na salama kutoka mapato ya ushuru wa mafuta na kwa kutumia mfumo wa “development finance” ili kumaliza kabisa tatizo la maji safi na salama.

- iv. Itawezesha Ujenzi wa barabara ya Korosho (**cashew ring road**) [Nangurukuru – Liwale – Nachingwea – Masasi – Newala – Tandahimba – Mtwara – Lindi – Nangurukuru] kutokana na mapato ya ushuru wa korosho kwa kutumia mfumo wa “development finance” ili kufungua wilaya zinazolima korosho na kufungua Wilaya ya Liwale kwa kufungua barabara za Songea-Liwale na Liwale-Morogoro.
- v. Itasimamia uwekezaji wa eneo maalumu la kiuchumi la Bagamoyo ili kuifanya Tanzania kuwa kituo cha usafirishaji wa majini katika Afrika na eneo la maziwa makuu na kuongeza ajira na mapato ya fedha za kigeni.
- vi. Itasimamia kukamilika kwa Uwekezaji wa kinu cha kuchakata gesi asilia (LNG) ili kuongeza mapato ya fedha za kigeni, ajira na maendeleo ya viwanda nchini.
- vii. Itasimamia kukamilika kwa Uwekezaji wa mradi wa uchimbaji madini ya Nikeli katika eneo la Kabanga, wilayani Ngara, mkoani Kagera.
- viii. Itafanya uchambuzi wa kina kwa miradi inayoendelea sasa, kama vile mradi wa Reli ya Kati (SGR), Mradi wa Umeme wa Maji Mto Rufiji (Nyerere|Stiglers Gorge), na Ufufuaji wa Shirika la Ndege la Taifa (ATCL). Kwa kutumia wataalamu wa ndani na wa nje, Serikali yetu itapata ushauri wa kitaalam kuhusu namna bora ya kutekeleza miradi mikubwa kwa ubia kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma, kwa kuzingatia muda wa miradi husika kuanza kuzalisha mapato ya kulipia madeni ya ununuzi/ujenzi wake. Lengo la uchambuzi huu ni kuiondoa Serikali kwenye angalau 50% ya gharama za utekelezaji ili kuelekeza rasilimali fedha kwenye miradi ya huduma za jamii, kama elimu, maji na afya, na kwenye miradi itakayochochea maendeleo ya watu, kama kilimo cha umwagiliaji.



4.11. Kulinda Mazingira

Mazingira ndiyo uhai wa taifa hili. Hivyo, Serikali ya ACT Wazalendo itahakikisha kuwa;

- i. Shughuli zote za maendeleo zinaheshimu, kuhifadhi na kulinda mazingira.
- ii. Inaheshimu mikataba yote ya kimataifa ya kulinda mazingira ikiwemo Mkataba wa Makubaliano ya Uhifadi Mazingira ya Paris (Paris Agreement), na tutaungana na mataifa mengine kuhakikisha mazingira yanalindwa kote duniani na kuhakikisha vijana na wanawake wanashiriki kikamilifu kwenye majukwaa ya kimataifa ya majadiliano.

- iii. Inapunguza hewa ya ukaa na matumizi ya plastiki.
- iv. Inawezesha NEMC kuwa shombo kinachofanya kazi kwa karibu na idara zote muhimu za Serikali.
- v. Makampuni na viwanda vikubwa wanachangia kupitia CSR mfuko wa ruzuku wa miradi ya kulinda mazingira.
- vi. Elimu ya asili ya utunzaji mazingira, inahifadhiwa na kutumika katika shughuli mbali mbali za kutunza mazingira.



4.12. Sera za Kodi

Ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo iliyoainishwa na kutoa huduma za jamii zilizo bora zitahitajika Fedha za kutosha. Pamoja na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika baadhi ya miradi, mapato ya ndani yatahitajika kugharamia sehemu kubwa ya maendeleo ya watu wetu na uendeshaji wa Serikali. **Katika kipindi cha Miaka Mitano Jumla ya Shilingi Trilioni 158 zitapatikana kutoka Mapato ya ndani.**

Serikali itakayoongozwa na ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

- i. Itaboresha mazingira ili kukuza shughuli za uchumi, kupanua wigo wa kodi na kuingiza watu wengi zaidi kwenye kulipa Kodi ili kufikia lengo la uwiano wa mapato ya Kodi kwa Pato la Taifa (Tax/GDP ratio) kufikia 25% ifikapo mwaka 2025.
- ii. Itaweka vivutio vya kikodi ili kuwezesha sekta binafsi kujenga miundombinu wezeshi na muhimu kwa mfumo wa ubia. Hii itaipa Serikali pumzi ya kujielekeza kwenye kutoa huduma muhimu kwa wananchi, kuepuka kuongeza Deni la Taifa na kukuza sekta binafsi.
- iii. Itatunga sera za kikodi ili kuhami sekta ya Utalii na mnyororo wake ambao umeathirika sana na janga la Covid 19. Hii ni pamoja na kulinda Ajira za Wafanyakazi wa Makampuni ya Utalii kwa kutoa ruzuku kwa kampuni zote zitakazoendeleza mikataba ya ajira na kuruhusu wafanyakazi waliokosa kazi kulipwa Fao la kukosa Kazi kutoka Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

- iv. Itaweka vivutio vya kibajeti na kikodi kwenye Miradi yote ya Kilimo cha Umwagiliaji na Viwanda vyote vya kuongeza thamani ya mazao ya Kilimo.
- v. Itarekebisha muundo mzima wa makato kutoka kwenye mapato ya waajiri na wafanyakazi ili kuchochea matumizi kwenye uchumi, kwa kupunguza PAYE kima cha chini mpaka asilimia nane (8%) kutoka asilimia tisa (9%) ya sasa.
- vi. Itafanya marekebisho ya Tozo ya kuongeza Ujuzi (Skills Development Levy) kwa kupanua wigo wa makusanyo kuhusisha sekta ya Umma na kushusha kiwango cha malipo mpaka 2% tu.
- vii. Itapunguza makato ya Bima ya Afya, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi WCF mpaka asilimia kumi na mbili (12%) kutoka asilimia ishirini na tatu (23%) ya sasa. Hivyo kupunguza jumla ya makato kutoka asilimia thelathini na mbili (32%) ya sasa mpaka asilimia ishirini tu (20%).
- viii. Itaimarisha sheria ya kuzuia ukwepaji wa Kodi wa Makampuni ya Kimataifa ili kuokoa Mapato sawa na 5% ya Pato la Taifa ambayo yanapotea kupitia mbinu za kahasibu zinazofanywa na Multinational Corporations. Kuwezesha hili Serikali itaingia mikataba ya kimataifa inayosadia mataifa kuzuia ukwepaji wa kodi.



5. GHARAMA ZA KUTEKELEZA ILANI

Ilani hii imetoa ahadi ambazo zitahitaji Fedha ili kutekelezwa. **Jumla ya Shilingi Trilioni 130** zitatakiwa kuwekezwa nchini ili kutekeleza miradi mikubwa ambayo itapelekea;

- Kuleta kilimo cha kimapinduzi na Vvwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, uvuvi na mifugo.
- Kuboresha huduma za jamii kama; afya, maji na elimu.
- Kujenga miundombinu wezeshi kama vile nishati ya umeme, barabara, reli na bandari
- Kuifanya Tanzania kufaidika na nafasi yake ya kijiografia kama kituo kikuu cha biashara na huduma katika eneo la Maziwa Makuu.
- Kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji mkubwa wa gesi asilia, chuma na bidhaa za chuma, Nikeli na bidhaa za nikeli na kufungamanisha sekta ya madini na sekta ya viwanda, kilimo, usafirishaji na nishati.

Baadhi ya vipaumbele vinavyohitaji Fedha nyingi ni pamoja na;

1. Gharama za elimu haswa upanuzi wa elimu msingi na elimu sekondari kutokana na kasi kubwa ya ongezeko la Wanafunzi **inayokadiriwa kufikia shilingi Bilioni 216 kila Mwaka kwa miaka 5**
2. Gharama za Elimu ya Ufundi na ya Juu haswa uamuzi wa Kufuta mikopo ya ada kwa Wanafunzi wa vyuo vya ufundi na vyuo vikuu **inayokadiriwa kufikia wastani wa shilingi Bilioni 600 kila Mwaka**
3. Gharama za Ujenzi wa VETA kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambazo **zinakadiriwa kufikia shilingi Bilioni 780 kwa miaka 5**
4. Uwekezaji wa vyuo vikuu vipya vya umma na gharama za ujenzi wa vyuo vya ufundi mchundo kwenye 50% ya Mikoa ya Tanzania Bara **inayokadiriwa kufikia shilingi Trilioni 3.4 kwa miaka 5**
5. Gharama za kuchangia Hifadhi ya Jamii kwa watu walio nje ya sekta rasmi (**matching funds**) ili kila Mtanzania kuwa na Bima ya Afya **inayokadiriwa kufikia shilingi Bilioni 648 kila mwaka**
6. Gharama za ujenzi wa hospitali kubwa 3 **zinazokadiriwa kufikia shilingi Bilioni 600 kwa miaka 5**

7. Gharama za mradi kabambe wa kusambaza maji kwa wananchi wote **inayokadiriwa kufikia shilingi Trilioni 10 kwa miaka 5**
8. Gharama ya ujenzi wa barabara ya korosho (Cashew Ring Road) **inayokadiriwa kufikia Shilingi Bilioni 700 kwa miaka 5**
9. Gharama za ujenzi wa skimu kubwa 5 za umwagiliaji wa jumla ya hekta milioni moja **zinazokadiriwa kufikia shilingi Trilioni 2.5 kwa miaka 5**
10. Gharama ya mradi wa Mchuchuma na Liganga **zinazokadiriwa kufikia USD 3.2 Bilioni** na reli ya Mtwara – Ludewa **inayokadiriwa kufikia shilingi Trilioni 1.2 kwa miaka 5**
11. Gharama ya mradi wa LNG Lindi **inayokadiriwa kufikia USD 30 Bilioni**
12. Gharama ya mradi wa Kabanga Nickel **inayokadiriwa kufikia USD 2 Bilioni** na reli ya Isaka-Ngara **inayokadiriwa kufikia shilingi Trilioni 1 kwa miaka 5**
13. Gharama ya mradi wa eneo la uchumi Bagamoyo **inayokadiriwa kufikia USD 10 Bilioni** kwa miaka 5
14. Gharama za upanuzi wa bandari za Tanga, Mtwara na Kigoma **zinazokadiriwa kufikia shilingi Trilioni Moja kwa miaka 5**
15. Gharama za ujenzi wa vinu vya kuzalisha umeme wa gesi 1,800MW na umeme jua, upepo na maporomoko ya maji 2,100MW **zinazokadiriwa kufikia shilingi Trilioni Mbili**

Fedha za Uwekezaji huu mkubwa na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla zitatoka maeneo yafuatayo;

- Uwekezaji wa sekta binafsi katika miradi ya Mchuchuma na Liganga, kinu cha kuchakata gesi Lindi, mradi wa Kabanga Nickel, vinu za kuzalisha umeme kutoka gesi asilia na eneo la uchumi la Bagamoyo. Hii ni miradi itakayoingiza nchini Fedha za Kigeni (FDI) na kuongeza uwezo wa Nchi kupata mapato ya ndani. Wajibu wa Serikali utakuwa ni kuweka mazingira mazuri na sera zinazotabirika (stable fiscal regime).
- Gharama za elimu ufundi na elimu ya juu zitatokana na Tozo ya kuongeza ujuzi (Skills Development Levy) ambayo baada ya marekebisho ya kupanua wigo wa walipaji itakuwa na uwezo wa kukusanya shilingi Bilioni 470 kila mwaka na kuongezeka kulingana na kuongezeka kwa shughuli za Uchumi Nchini.

- Gharama za Ujenzi wa Miradi ya Maji zitagharamiwa na Tozo maalumu ya matumizi ya Mafuta ya Petroli. Serikali itachukua mkopo nafuu wa muda mrefu wa Shilingi Trilioni 10 kutoka Benki za Maendeleo ili kutekeleza mradi mara moja na mapato ya 'fuel levy' yatahudumia mkopo huo mpaka utakapomalizika kulipwa. Tozo ya shilingi 200 kwa kila lita ya Mafuta itazalisha Jumla ya shilingi Bilioni 700 kila Mwaka zinazoweza kutumika kulipa mkopo wa muda mrefu wa miaka 15.
- Gharama za Ujenzi wa Barabara ya Korosho (Cashew Ring Road) zitalipiwa na 50% ya mapato ya ushuru wa Korosho (exports levy) ambapo Serikali itachukua mkopo nafuu wa muda wa kati ili kupata fedha za ujenzi wa barabara hiyo mara moja na mapato ya exports levy yatahudumia mkopo huo mpaka utakapomalizika kulipwa. Ushuru wa Korosho unakadiriwa kuingiza mapato ya zaidi ya shilingi Bilioni 245 kila Mwaka ambazo nusu yake inaweza kulipa mkopo wa barabara hiyo na barabara za Songea-Liwale na Liwale-Morogoro kwa muda wa miaka 10
- Gharama za miradi mikubwa ya umwagiliaji zitalipiwa kutoka uwekezaji wa skimu ya Hifadhi ya Jamii kwa wakulima kama uwekezaji wa Skimu wa muda mrefu.
- Gharama nyengine zote zitaweza kulipwa na Serikali kutokana na mapato ya ndani ikiwemo kuongeza mishahara kwa watumishi wa umma ikiwemo madeni ya miaka 5 iliyopita, uboreshaji wa mfumo wa utoaji haki nchini (criminal justice system), kulipa madeni ya mapato ya Zanzibar kutoka mgawo wa mapato ya Muungano ambao haukuwa ukilipwa kwa miaka yote ya nyuma na fidia kwa watu wote waliobambikiwa kesi katika utawala wa awamu ya tano.



6. TANZANIA KUFIKIA 2025

Ifikapo mwaka 2025 Tanzania itakuwa na jumla ya watu milioni 71 kwa mujibu wa makadirio ya Umoja wa Mataifa. Serikali yetu itakuwa inakabiliana na jukumu la kuongeza shughuli za kiuchumi ili kukidhi haja ya ongezeko la watu, vijana wanaotaka ajira nyingi na bora na huduma muhimu kama Elimu na Afya.

Baada ya miaka mitano ya Uongozi wa Serikali ya ACT Wazalendo, na utekelezaji wa Sera zetu katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar, tunataka Taifa letu liwe na matokeo yanayotupelekea kwenye uchumi unaokua, uliochangamka na unaoelekea kuwa jumuiifu ambapo;

- Wastani wa pato la mtu mmoja litakuwa Dola za Marekani 1,300.
- Watanzania wanaoishi chini ya mstari wa umasikini kuwa 14% tu,
- Ukosefu wa ajira kuwa chini ya 8%, na
- 60% ya watu wote wanaojihusisha na shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji na biashara ndogo zilizosajiliwa wamekuwa na Hifadhi ya Jamii na wananchi wote kuwa na Bima ya Afya
- Haya yatakuwa ni matokeo ya Sera na mikakati ambayo katika miaka mitano 2020-2025 itafanikisha;
- Uwekezaji katika uchumi wa vijijini (rural economy), kupitia ushirika wa kisasa (Community Wealth Building) ambao utawezesha mapinduzi ya kilimo na kuongeza thamani mazao ya kilimo na hivyo kuwezesha sekta ya kilimo kukua kwa kasi ya 8-10% kwa mwaka kuanzia mwaka 2022.
- Uwekezaji kutoka nje katika sekta zote za uchumi na kuifanya Tanzania kuwa nchi inayoongoza kupokea uwekezaji (FDI) katika eneo la Maziwa Makuu.
- Uwekezaji katika elimu ya msingi, elimu ya ufundi (kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuwa na Chuo cha VETA) na 50% ya Mikoa ya Tanzania Bara kuwa na chuo cha ufundi na elimu ya juu kwa kuwa na vyuo vikuu vipya vya Taifa vitano (vitatu Tanzania Bara – Mtwara, Kigoma na Tanga, na viwili Zanzibar – Pemba na Unguja) vyenye wanafunzi 20,000 kila kimoja.
- Uwekezaji katika afya kwa kuwa na hospitali kubwa 3 za Kanda; katika kanda ya ziwa- (Mara), Nyanda za juu kusini (Ruvuma) na Kanda ya kati (Singida) zenye uwezo, ukubwa na viwango vya kimataifa kwenye kutoa huduma. Kutokana na Hifadhi ya Jamii kila Mtanzania kuwa na Bima ya Afya.
- Uboreshaji wa muundo wa Muungano kufuatia kupitishwa kwa Katiba mpya: Muungano wa Serikali Tatu na wenye Usawa, Haki na wa kuheshimiana.
- Serikali za Mitaa kuwa na uhuru wa kupanga maendeleo ya watu wao na kuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato.
- Kuwa na Serikali za Mikoa ambazo wananchi wanawachagua wakuu wa mikoa kuanzia uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

SURA YA TANZANIA KITAKWIMU OKTOBA 2025

#KAZINABATA

IDADI YA
WATANZANIA

MILIONI

71



PATO LA
TAIFA

BILIONI



92.3



UKUAJI WA UCHUMI

11%

MAUZO YA NJE USD 'BILIONI'





SAFARI YA KUREJESHA FURAHA IMEANZA. KARIBU Nawe USHIRIKI.

Kazi tuliyonayo si ya mtu au kikundi kimoja.
Ni jukumu letu sote. Sio suala la utajiri au kipato
kikubwa. Ni suala la moyo wenye matumaini ya
kurejesha raha na ndoto zilizovunjika. Kwa moyo
na ushirika mmoja - **WOTE TUNaweZA.**



NMB (T) Ltd

Mikocheni Branch

A/c Name: **ACT WAZALENDU UCHAGUZI**

A/c Number: **22610026136**

Swift Code: **NMIBTZTZ**



Mpesa

A/c Name: **ACT Wazalendo**

PhoneNumber: **+255 744 959112**



Kupitia Tovuti

www.actwazalendo.or.tz/donation_options

P.O. Box 105043, Dar es salaam | info@actwazalendo.or.tz
www.actwazalendo.or.tz | +255 712 622642 / 653 619906